KUCHUNGUZA KIWANGO CHA MABADILIKO YA MATUMIZI YA MSAMIATI WA KIPEMBA

KAUTHAR ABDALLA SULEIMAN

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MASHARTI YA DIGIRII YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

KUCHUNGUZA KIWANGO CHA MABADILIKO YA MATUMIZI YA MSAMIATI WA KIPEMBA

KAUTHAR ABDALLA SULEIMAN

IMEWASILISHWA IKIWA NI SHARTI PEKEE LA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo: **Kuchunguza Kiwango cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati wa Kipemba** na ameridhika kwamba tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A. Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…….…….

Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

…….

Tarehe

HAKIMILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii, hairuhusiwi kukaririwa au kuhifadhiwa kwa njia yoyote au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu katika hali yoyote ile bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Kauthar Abdalla Suleiman,** natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo *"Kuchunguza Kiwango cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati wa Kipemba"* ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa na wala haitahudhurishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada kama hii.

……

Saini

……

Tarehe

TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazee wangu ambao wameshafika mbele ya haki: Mama yangu Asha Alawy Omar na baba yangu Abdalla Suleiman Hamad. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao pahali pema peponi.

AMIIN

SHUKURANI

Mwanzo kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, kwani yeye ndiye mstahili na ndiye aliyenipa uwezo wa kuikamilisha kazi hii, hakika bila yeye hapana kinachokuwa. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa kila mmoja aliyetoa msaada wa hali na mali katika kuifanya kazi hii hadi ikakamilika.

Hata hivyo, hapa nitawataja watu wachache tu, ambao kwa kiwango kikubwa wametoa mchango wao katika kufanikisha kazi hii. Kwanza kabisa natoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dkt. Zelda Elisifa, kwa uvumilivu, busara na imani ya kunipa moyo wa kuendelea na kazi hii pamoja na upendo wake mkubwa alionionesha wakati wote alipokuwa akinisaidia kimawazo na kimaelekezo ambayo yamejenga msingi wa utafiti wangu. Pili napenda kumshukuru sana Professa Tigiti Sengo, Dkt. Peter Lipembe pamoja na Dkt. John Msindai, wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Makao Makuu Dar-es-salaam, kwa kutoa mchango wao mzuri kipindi chote ambacho mtafiti alikuwa akiiwasilisha kazi hii. Vilevile sitomsahau Dkt. Maulid Haji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ushirikiano wake wa dhati katika kutoa miongozo kwa lengo la kuleta ufanisi wa kazi hii.

Shukurani ziwafikie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kuniruhusu kusoma bila ya pingamizi yoyote pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar.

Pia nawashukuru masheha wote wa vijiji vya Kojani, Kiuyu, Mkungumalofa na Kiwani Nanguji kwa kunipeleka kwa wanavijiji kwa lengo la kukusanya taarifa

zilizosababisha kukamilika kwa utafiti huu. Pamoja na wao, namshukuru Bi Saumu Abdalla Suleiman, Bwana Hamad Magarawa pamoja na Bimkubwa Hamad Magarawa kwa kunipeleka na kuniongoza kufika maeneo yote yaliyotafitiwa.

Vilevile shukurani za pekee kwa mume wangu Hamad Hassan Omar, watoto wangu Badria (Queen) Hamad Hassan na Hussam Hamad Hassan kwa uvumilivu waliokuwa nao pamoja na kuhimili hali ya upweke na hasa kipindi chote nikiwa nje ya Zanzibar kwa ajili ya utafiti huu. Kwa wote napenda kuwatakia kheri, mafanikio na baraka kwao binafsi, kwa nchi yetu ya Zanzibar, Tanzania na pia kwa maendeleo ya Afrika kwa ujumla.

IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo la “Kuchunguza Kiwango cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati wa Kipemba katika Muktadha wa Harusini, Msibani, Uvuvini na Kilimoni”. Malengo ya utafiti yalikuwa; (i) Kuainisha msamiati wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni unaotumika katika lahaja ya Kipemba. (ii) Kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo. na (iii) kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Foucault (1981) ya Mwenendo na Mabadiliko. Nadharia ya Darwin (1838) ya Ubadilikaji na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) ya Giles ya mwaka (1991). Jumla ya watafitiwa 87 walishiriki katika utafiti huu. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, usaili na maelezo. Pia data ziliainishwa kwa njia ya kiidadi (kitakwimu) na isiyo ya kiidadi (maelezo). Utafiti umeonesha kuwa; (i) Msamiati wa muktadha wa harusini umebadilika zaidi kuliko miktadha mingine mitatu sawa na 33.33%. (ii) Msamiati wa kilimoni na uvuvini ukifuatia sawa na 22.81% kwa kila muktadha. (iii) Utafiti umegundua kuwa msamiati wa msibani umebadilika kwa kiwango kidogo wastani wa 21.05%. Sababu za mabadiliko hayo tafiti imeonesha ni kukua kwa sayansi na teknolojia, matumizi ya utandawazi pamoja na vyombo vya mawasiliano, kuwepo kwa lahaja iliyorasmi, athari ya maendeleo ya watu kuhamahama, mabadiliko ya kiutamaduni, maingiliano ya kindoa na misimamo ya kidini. Utafiti huu unapendekeza, msamiati wa Kipemba uendelee kutumika kwani unasaidia kuwatambua watu wenye asili hiyo na kujaza pengo la istilahi za Kiswahili na msamiati wa Kipemba ni amana na hazina ya lugha yetu uhifadhiwe vizuri ili amana hii ya lugha isipotee.

YALIYOMO

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO LA MTAHINIWA ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

MAJEDWALI ..... **xii**

VIELELEZO ..... **xiii**

VIAMBATANISHO ..... **xiv**

VIFUPISHO VYA MANENO ..... **xv**

SURA YA KWANZA **1**

1.0 UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa Mada 1

1.1.1 Sababu Zinazosababisha Kutokea kwa Lahaja 3

1.2 Tatizo la Utafiti 5

1.3 Malengo ya Utafiti 5

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti 5

1.3.2 Malengo Maalumu ya Utafiti 6

1.4 Maswali ya Utafiti 6

1.5 Umuhimu wa Utafiti 6

1.6 Muhtasari wa Sura 7

SURA YA PILI **8**

2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA ZA UTAFITI **8**

2.1 Utangulizi 8

2.2 Utalii wa Kazi Tangulizi 8

2.2.1 Lugha ya Kiswahili 8

2.2.2 Lahaja Mbalimbali za Kiswahili 13

2.2.3 Lahaja ya Kipemba 21

2.3 Pengo la Utafiti 28

2.4 Mkabala wa Kinadharia 29

2.4.1 Nadharia ya Mwenendo na Mabadiliko 29

2.4.2 Nadharia ya Ubadilikaji 30

2.4.3 Nadharia Kidhi ya Mawasiliano 31

2.5 Muhtasari wa Sura 31

SURA YA TATU 32

3.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI 32

3.1 Utangulizi 32

3.2 Mbinu za Kukusanyia Data 32

3.2.1 Njia ya Hojaji 32

3.2.2 Njia ya Usaili 33

3.2.3 Njia ya Maelezo 33

3.3 Mipaka ya Utafiti 34

3.4 Mbinu za Usampulishaji wa Watafitiwa 34

3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji wa Data 35

3.6 Mbinu za Kuchambua na Kuchanganua Data 36

3.7 Muhtasari wa Sura 37

SURA YA NNE 38

4.0 UCHAMBUZI WA DATA 38

4.1 Utangulizi 38

4.2 Uainishaji wa Msamiati 39

4.2.1 Msamiati wa Harusini 39

4.2.2 Msamiati wa Msibani 47

4.2.3 Msamiati wa Uvuvini 54

4.2.4 Msamiati wa Kilimoni 60

4.3 Kutathmini Tofauti ya Kiasi cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati Kiasilimia 67

4.3.1 Uchambuzi 68

4.4 Kuchunguza Sababu Zilizosababisha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati 71

4.4.1 Sababu za Kiuchumi 72

4.4.2 Sababu za Kijamii 73

4.5 Muhtasari wa Sura 77

SURA YA TANO 78

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 78

5.1 Utangulizi 78

5.2 Muhtasari 78

5.2.1 Muhtasari wa Ujumla 78

5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 80

5.3 Mapendekezo ya Utafiti 82

MAREJELEO 84

VIAMBATANISHO 90

MAJEDWALI

Jedwali Na. 2.1: Idadi za Lahaja ya Kiswahili 14

Jedwali Na. 2.2: Aina za Lahaja ya Lugha ya Kiswahili 15

Jedwali Na. 2.3: Tofauti ya Msamiati kati ya Kenya naTanzania 16

Jedwali Na. 2.4: Idadi ya Lahaja ya Kipemba 22

Jedwali Na. 2.5: Tofauti ya Vitamkwa vya Mofimu katika Msamiati 24

Jedwali Na. 2.6: Maneno ya Kipemba na Kiswahili Fasaha 26

Jedwali Na. 3.1: Idadi na Matabaka ya Watafitiwa 35

Jedwali Na. 4.1: Msamiati Unaotumika Kabla ya Harusi 40

Jedwali Na. 4.2: Msamiati Unaotumika Wakati wa Harusi 43

Jedwali Na. 4.3: Msamiati Unaotumika Baada ya Harusi 46

Jedwali Na. 4.4: Msamiati Unaotumika Kabla ya Msiba..... 49

Jedwali Na. 4.5: Msamiati Unaotumika Wakati wa Maziko 51

Jedwali Na. 4.6: Msamiati Unaotumika Baada ya Msiba 53

Jedwali Na. 4.7: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Samaki 55

Jedwali Na. 4.8: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Vitu vya Uvuvini 57

Jedwali Na. 4.9: Msamiati Unaotumika Kuonesha Vitendo vya Uvuvini 59

Jedwali Na. 4.10: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Mimea..... 62

Jedwali Na. 4.11: Msamiati Unaotumika katika Majina yaVitu vya Kilimoni..... 64

Jedwali Na. 4.12: Msamiati Unaotumika KuoneshaVitendo vya Kilimoni..... 66

Jedwali Na. 4.13: Sababu Zilizosababisha Mabadiliko katika Lahaja ya Kipemba .. 72

VIELELEZO

Kielelezo Na. 4.1: Tofauti ya Mabadiliko ya Msamiati 68

Kielelezo Na. 4.2: Tathmini ya Mabadiliko ya Msamiati Kiujumla 70

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho I: Maswali ya Hojaji kwa Vijana 90

Kiambatanisho II: Maswali ya Mazungumzo kwa Ajili ya Wazee..... 92

VIFUPISHO VYA MANENO

Agh.	Aghalabu
BAKITA	Baraza la Kiswahili Tanzania
BAKIZA	Baraza la Kiswahili Zanzibar
BBC	British Broadcasting Cooparation
CD	Compact Disk
Chake	Chakechake
CMS	Church Missionary Society
Juml	Jumla
Kisw/ Sanifu	Kiswahili Sanifu
Kiw cha Mab	Kiwango cha Mabadiliko
M/Malofa	Mkungumalofa
M/weni	Micheweni
NKM	Nadharia Kidhi ya Mawasiliano
SUZA	State University of Zanzibar
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (kwa sasa TATAKI - Taasisi ya Taalimu za Kiswahili
UMCA	Universities Mission to Central Africa
Uk	Ukurasa
WK	Wanawake
WM	Wanaume

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Kipemba ni lahaja inayozungumzwa kisiwani Pemba. Ni moja wapo miongoni mwa lahaja ya lugha ya Kiswahili. Naye Senkoro (1988) amesema neno Kiswahili linatokana na neno la Kiarabu, sahil lenye maana ya upwa. Mekacha (keshatajwa) alisema Kiswahili ndio lugha ya dola na ya kijamii yenye mawasiliano mapana yaliyoenea katika jamii za watu wote wa Afrika Mashariki na Bahari ya Hindi na hadi kuwa lugha za jamii nyingine kote kilikopendwa. Kwa upande wa visiwa vya Zanzibar (Unguja na Pemba), Kiswahili ni lugha ya kwanza (lugha mama) kwa wenyeji wake wote. Hii ina maana kuwa wazaliwa wa visiwa hivyo hawana lugha ya kikabila zaidi ya Kiswahili. Masebo na Nyangwine (2004), wamefasili lugha mama ni lugha ambayo mtu hujifunza utotoni mwake wakati anakua kabla ya kujifunza lugha ya pili. Ingawa Kiswahili cha Wazanzibar hao kimetofautiana. Mhilu (2010) amesema licha ya kuwa Kiswahili ni lugha kuu moja lakini watumiaji wa eneo moja hutofautiana na watumiaji wa eneo jingine katika msamiati, matamshi, muundo na maumbo. Mabadiliko hayo hudhihirisha kuwepo kwa lahaja.

Farlex (2003 - 2015) kupitia Mtandao wa *www.thefreedictationary.com/dialects* umesema lahaja kwa Kiingereza ni **dialect**, neno ambalo lina asili ya maneno mawili ya Kigiriki ambayo ni **dia** (kupitia) na **legein (**uzungumzaji). Katika karne ya 16, Waingereza walilitumia neno **dialect** (lahaja) lenye maana ya namna mbalimbali za kusema.

Dhana ya lahaja si ngeni ulimwenguni na hasa kwa wanaisimu lakini inawezekana ikawa ni ngeni Uswahilini (sehemu ambazo wanajamii wake wanaitumia lugha ya Kiswahili katika kuwasiliana kwao), kwa jamii zote zinazotumia lahaja hizo za Kiswahili. Kwa sababu kila jamii ndogo, lahaja inayozungumzwa pao ndio lugha yao kamili. Mfano: Makunduchi, watakwambia lugha yetu ni Kimakunduchi, Kojani - Kikojani, Tumbatu - Kitumbatu, Walamu - Kilamu, na kwingineko, hawasemi kuwa tunazungumza Kiswahili cha lahaja ya Kimakunduchi, Kikojani au Kitumbatu.

Zipo fasili nyingi zinazofafanua dhana ya lahaja. TUKI (2004) imeandika lahaja ni tofauti ya matamshi, maumbo na matumizi ya maneno mbalimbali kwa lugha yenye asili moja. Mkude (1993) amesema lahaja ni usemaji unaoangukia katikati ya usemaji wa mtu binafsi na usemaji wa jamii ya lugha moja. Tuli (1985) ameeleza kuwa lahaja ni vilugha vya maeneo katika jamii inayotumia lugha kubwa moja. Wamitila (2003) amesema ni lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha watu ambao huonesha tofauti za maneno, maumbo, matamshi na aina nyingine za lugha fulani. Kwa ufupi lahaja ni mfumo kamili wa mawasiliano unaotumiwa na jamii moja ukitofautiana na jamii nyingine katika uzungumzaji wa wasema lugha kuu yenye asili moja. Masebo na mwenzake (2004) wamesema hakuna lugha wala lahaja iliyo bora zaidi ya nyingine na isitokee lahaja yoyote kuonekana dhaifu au duni.

Kwa upande wa msamiati Chum (keshatajwa) hakuhitilafiana na Kiango na wenzake (2009), wao wamesema msamiati ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha na TUKI (ishatajwa), imeeleza kuwa msamiati ni jumla ya maneno katika lugha. Kwa hiyo msamiati ni maneno yote yanayopatikana au yanayotumiwa na watu katika lugha husika. Pia TUKI (imeshatajwa) imesema mabadiliko ni hali inayokuwepo

baada ya kutokea mageuzi fulani. Fasili ya Kipemba kutoka Taasisi ya Elimu (ishatajwa) inayoshughulikia elimu na mitaala ya Tanzania na Said (2011) wote hao wamesema Kipemba ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Tunaweza kusema kwamba Kipemba ni lahaja yenye asili ya wazawa wa kisiwa cha Pemba. Wapemba hao hata kama wapo nje ya kisiwa cha Pemba wanaweza kuzungumza Kipemba chao ingawa kwa sasa kumejitokeza mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo.

1.1.1 Sababu Zinazosababisha Kutokea kwa Lahaja

Masebo na Nyangwine (2004) na Mhilu (2010) wamesema kuwa zipo sababu mbili kuu zinazosababisha kuzuka kwa lahaja nazo ni:

(i) Sababu za Kijiografia (Maeneo tofauti ya wazungumzaji).

Wazungumzaji wa lugha moja huweza kutawanyika katika maeneo tofauti, pingine kwa matakwa yao binafsi kama ya kibiashara, kindoa, kikazi na sababu nyinginezo au hata kutenganishwa na maumbile ya kijiografia, mfano: kisiwa, mito, bahari na mipaka ya kinchi. Udhaifu wa sababu hii ni kuwa watu waliotawanyika wakiwa ni watu wazima ni vigumu kubadilika na hata kama watabadilika basi ni kwa kiwango kidogo tu.

(ii) Sababu za kijamii na uchumi (ngazi za kiuchumi, matabaka ya kijamii na ushawishi wa kimakundi).

Hii inatokana na kuibuka kwa matabaka ya kijamii, ngazi ya elimu na kazi, umri, mazingira ya nyumbani na malezi. Kwa kawaida watu wa kipato cha chini au wenye elimu duni hutumia zaidi lugha isiyorasmi na lahaja zao wakati wenye kipato cha juu

hutumia lugha rasmi. Hata hivyo mabadiliko yatokeayo upande mmoja si lazima yajitokeze sehemu nyingine. Naye Khamis (1984:63) amechangia swali hili kwa kusema “Mabadiliko yanalazimisha kuchunguzwa kwa lahaja na vilugha vyake, tofauti ya maendeleo (kijamii, kiuchumi na kiutamaduni) baina ya mji na vijiji inasababisha muingiliano na hatari ya mabadiliko ya lughawia kutoka sehemu moja kwenda nyingine”. Juma (2006) ameeleza kuwa usahihi wa mipaka ya lahaja unaweza kubadilika kutokana na athari za maendeleo ya kiuchumi, na mambo mingine ya kijamii kama kuhamahama, kuoana, mgawanyo wa kiutawala mfano wilaya, shehia, mkoa, na mingineyo. Kipacha (2003) amesema kuwa msambao wa wazungumzaji na jinsi lugha waitumiayo inavyobadilika huwa ndio chanzo cha kuzuka kwa tofauti ndogondogo tunazoziita lahaja. Pia Nyangwine (2001) ameyaorodhesha mambo yanayosababisha lahaja kutokea (chanzo cha lahaja) kama yafuatayo:

(i) Umbali wa kijiografia kutoka eneo moja hadi jingine.

(ii) Kutawanyika kwa watu (kuhamahama kwa watu).

(iii) Kuingiliana na kuoana kwa watu (mwingiliano wa tamaduni tofauti).

(iv) Biashara mbalimbali.

(v) Dini.

(vi) Elimu na siasa, husababisha kuwepo kwa matabaka ya watu katika jamii (tabaka la juu, wasomi na viongozi) na tabaka la chini.

Kwa ufupi, wanaisimu hawakuwa na mawazo yanayopingana kihoja juu ya uzukaji wa lahaja katika jamii za wazungumzaji wa lugha moja. Hivyo uzukaji wa lahaja hauwezi kuepukika wala kuzuilika kwani lahaja ndizo zinazoikuza lugha.

1.2 Tatizo la Utafiti

Kipemba ni miongoni mwa lahaja maarufu sana katika lahaja za Kiswahili. Mwananadharia Tabouret (1989) amesema kuwa utambulishi wa mtu umefungamana na mambo mingi kama vile lugha, utamaduni, mila na desturi, mavazi, chakula, dini, historia za jamii, siasa na kiuchumi. Hata hivyo kumejitokeza athari za usasa katika lahaja hiyo ambayo imesababisha mabadiliko mbalimbali ya matumizi ya msamiati wa lahaja hiyo, iliyopelekea kuvia kwa matumizi yake. Miktadha mbalimbali ya matumizi ya msamiati huo imebadilika na mingine imefuawa na baadhi imekufa kimatumizi.

Khatib (2010) amesema kijuujuu inaonekana kuwa zimebakia sehemu za ndani sana za Pemba ambazo bado zinatumia msamiati asilia wa lahaja hizo. Hivyo yapo maswali kadhaa mtu anaweza kujiuliza. Lahaja hii imegubikwa na nini? Ni msamiati upi uliobadilika? Muktadha upi wa msamiati unabadilika zaidi kuliko miktadha mingine? Kwa sababu zipi au kwa nini msamiati huu ubadilike? Kutokana na tatizo hilo, mtafiti amekusudia kuubainisha msamiati uliyobadilika kutoka katika asili yake pamoja na sababu zilizosababisha mabadiliko hayo katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni. Hili ni tatizo zito linalohitaji kutatuliwa kitaalimu ili kuibainishia jamii kuwa Kipemba kinachozungumzwa hivi sasa kimebadilika ama hakijabadilika kama inavyoaminika na watu wingi.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Kuchunguza kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba ambao unatumika katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

1.3.2 Malengo Maalumu ya Utafiti

1.3.2.1 Kuuainisha msamiati wa Kipemba ambao umebadilika matumizi yake katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

1.3.2.2 Kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia kwa kila muktadha husika.

1.3.2.3 Kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo.

1.4 Maswali ya Utafiti

1.4.1 Ni msamiati gani wa Kipemba ambao umebadilika matumizi yake katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni?

1.4.2 Kuna tofauti gani ya mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba kiasilimia kulingana na muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni?

1.4.3 Ni sababu zipi zilizochangia kuleta mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umeweka wazi uwanja wa msamiati na mabadiliko yake katika lahaja za Kipemba. Pia utawashawishi watafiti wingine kuchunguza na kuandika tasnifu, kamusi na vitabu kwa lengo la kuhifadhi na kuiendeleza lugha ya Kiswahili kupitia lahaja ya Kipemba. Vilevile utatoa mchango kwa wanajopo wa hifadhi ya lugha ya Kiswahili, katika kutengeneza kamusi moja la lugha yao bila ya kutaja lahaja, kwa vile jiti moja kubwa la Kiswahili litakuwa limesimamishwa na lahaja, zikiwa ndizo mizizi.

1.6 Muhtasari wa Sura

Sura hii imetoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ambayo ni "Kuchunguza Kiwango cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati wa Kipemba". Kwanza imeeleza usuli wa mada pamoja na tatizo la utafiti. Vilevile imeonesha lengo kuu la utafiti, malengo maalumu ya utafiti na maswali ya utafiti. Sura hii imemalizia kwa kueleza umuhimu wa utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA ZA UTAFITI

2.1 Utangulizi

Katika kipengele hiki mtafiti alitalii machapisho na tafiti mbalimbali katika vitabu, makala, tasnifu, pamoja na mitandao ili kupata mawazo na maarifa yaliyotangulia juu ya mada aliyokuwa akiitafiti. Pia inafafanua kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

2.2 Utalii wa Kazi Tangulizi

Utalii huu ulihusisha maeneo matatu, kazi tangulizi zinazohusu lahaja mbalimbali za Kiswahili, lugha ya Kiswahili kiujumla na lahaja ya Kipemba.

2.2.1 Lugha ya Kiswahili

Hizi ni kazi ambazo zinahusu lugha ya Kiswahili kwa ujumla, umuhimu wa msamiati asilia wa Kiswahili, uwezo wa Kiswahili pamoja na njia mbalimbali za kuunda msamiati katika lugha ya Kiswahili.

Zipo fasili nyingi zinazoelezea maana ya lugha. Mhina na Kimbila (1971) wamefasili lugha, kuwa ni mfumo wa sauti za kusemwa ambazo huiwezesha jumuia ya watu wa utamaduni fulani wapashane habari. Mfaume (1984) amesema lugha ni utaratibu maalumu wa sauti za kusemwa na za nasibu zinazotumika na jamii ya utamaduni wa watu fulani katika kupashana habari au kuwasiliana. O'Grady na wenzake (1997) wameeleza kuwa kipaji cha lugha ndicho kinachomtofautisha binaadamu na viumbe wingine. Kwa mujibu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (1996), lugha ni ile ya kusema

au kuzungumza na maandishi ni kitambulishi cha lugha. Kwa hivyo, lugha ni utaratibu au mfumo wa sauti za nasibu zinazotamkika ambazo zina maana na hutumiwa na binaadamu kwa madhumuni ya mawasiliano miongoni mwao.

Duniani zipo lugha za aina mbalimbali. Nyingi kati ya hizo zimebeba majina ya nchi zao. Mekacha (1993) amebainisha ukweli huo kwa kutoa mifano, Kiingereza - Uingereza, Kichina - Uchina, Kisomali - Somalia, Kiswahili - Nchi za mwambao wa Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania, Uganda). Chum (1994) amesema Kiswahili ni miongoni mwa lugha maarufu sana na yenye wazungumzaji wingi ulimwenguni kote. Kwa maelezo ya BAKITA (1976) lugha ya Kiswahili inashika nafasi ya saba katika lugha kuu za dunia. Ni dhahiri kwamba Kiswahili kimeenea na kukua ulimwenguni kote. Ukweli wa hayo, Simala (2002) kazitaja idhaa mbalimbali za radio na runinga ambazo huandaa baadhi ya vipindi kwa lugha ya Kiswahili ulimwenguni. Kwa mfano: BBC, Radio Cairo, The Voice of America, Radio Sudan, Radio Japan international, Radio Deutschwelle, Radio China International, Radio South Africa na Radio Moscow International. Kwa maelezo ya Masebo na mwenzake (2004) Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha rasmi ya serikali mwaka 1925, wakati wa serikali ya Kiingereza ingawa katika shughuli za kiserikali kilikuwa Kiingereza kikitumika zaidi. Hata hivyo utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili haukuwa na nguvu kwa wakati huo. Maarifa ya wataalamu hao yamemsaidia mtafiti kuielewa maana ya lugha pamoja na historia ya lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Abdulaziz (1971) baada ya uhuru, raisi wa Jamhuri ya Muungano kwa wakati huo, Julias Kambarage Nyerere, alitangaza kuwa nchini Tanzania

Kiswahili ni lugha rasmi kwenye hotuba yake ya tarehe 10/12/1962 kwenye sikukuu ya Jamhuri, baada ya hapo shughuli zote za kiserikali zikaanza kutekelezwa kwa lugha ya Kiswahili zikiwemo za kiofisi, mikutano, shughuli za kimahakama na utoaji wa elimu ya msingi. Pia lugha hii iliteuliwa kuwa lugha ya Taifa mwaka 1964.

Tumbo na wenzake (1992) wameeleza kuwa baada ya Wamishionari kuwasili Tanganyika Januari 1844 kwa lengo la kueneza Injili, waliamua kutumia Kiswahili katika kazi hiyo na waliichagua lahaja ya Kiunguja mjini iwe lugha rasmi. Uchaguzi huo ulizua mjadala mkubwa baina ya kundi la Edward Steere wa madhehebu ya U.M.C.A (Universities Mission to Central Africa) kwa Zanzibar na J.C Krapf wa madhehebu ya C.M.S (Church Missionary Society) aliyekuwa akiishi Mombasa na wao walitaka Kimvita kiwe lugha rasmi.

Lakini makundi yote hayo yalikuwa ni wageni wa Kiswahili. Kwa wakati huo inaonekana hicho Kishangani mjini kilikuwa kikizungumzwa Malindi na Shangani tu, wakati historia inaonesha Zanzibar kulikuwa na miji ambayo ilikaliwa na wenyeji zaidi ambao walikuwa wakitumia lahaja zao mfano; Unguja Ukuu, Tumbatu na Kizimkazi.

Pia Sengo (2011:23) ameelezea uwezo na asili ya lugha ya Kiswahili, amedai kuwa “lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika ambazo zinajitosheleza kimsamiati, kimatamshi na ina sarufi yake”. Huyu anapinga mawazo ya kuwa Kiswahili hakijitoshelezi na hakiwezi kutumika katika elimu, Yeye amesema hayo ni mawazo ya kutawaliwa na ni utumwa wa mawazo. Pia ameendelea kusema, “Uswahili na mswahili ni kitambulishi cha watu (jamii) na kutunza uzalendo”.

Hata Honero na mwenzake (1978) walisema msamiati wa Kiswahili cha asili upo ingawa umeachwa kutumika na kupotea mfano wa baadhi ya msamiati huo ni:

Goni - jura/juha

Rahisi - mavuyo

Ngeu - damu

Penyenye/ngeya - nafasi

Pia Mwaro ameandika makala iliyoharirirwa na Mdee (2001) yenye mada ya utandawazi wa Kiswahili kwa kufuata msamiati wa zamani, amesema ufufuaji wa msamiati ni kuurudisha katika matumizi yake, msamiati ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu. Msamiati wa zamani upo lakini kwa sasa umesahaulika na hauandikwi, msamiati huo ulikuwa ukipatikana kwenye kamusi za zamani tu. Mfano; *Utenzi wa Mwanakupona,* uliotungwa miaka ya (1810 - 1820) na *Utenzi wa Tambuka uliyotungwa mwaka* (1810 - 1820). Pia akaonesha umuhimu wa msamiati wa zamani kuwa unaijenga na kuikuza lugha. Mfano wa baadhi ya msamiati huo ni:

Kiingereza	**Kiarabu**	**Asili ya Kibantu**
Venus	Zuhura	Yeyuni/kombeli
Earth	Ardhi/dunia	Ntozi/tiatizi

Vilevile akaonesha maneno yaliyosanifiwa kutoka Kiswahili cha asili na kusahaulika kuwa Kiswahili sanifu. Mfano: Kalamu - udandi, wakati - mwiya na chumvi - munyu.

Pia Mutiso (1992) ameeleza kuwa Kiswahili hakijawahi kuwa na pengo kubwa kimsamiati na aliona kuwa Kiswahili kinaweza kurudishwa ukale wake wa uasili

kwa kufufua na kuhuwisha maana ya maneno ya kilahaja. Mutiso (keshatajwa) amejaribu kutoa mifano mbalimbali ya maneno ya mkopo na Kiswahili cha asili mfano, kalamu - udandi, mkuki - fumo, damu - ngeu.

Pia kazi ya Kiango (1995) ilionesha mbinu mbalimbali za uundaji wa msamiati mpya katika Kiswahili. Yeye alisisitiza kuwa zoezi la kuunda msamiati sio la kipekee kwa Kiswahili bali ni uhai wa lugha zote duniani. Baadhi ya njia alizozionesha ni:

(i) Kukopa kwa kutohoa: Mfano, office - afisi, atom - atomi, fridge - friji, bicycle - baskeli.

(ii) Kukopa kwa kutafsiri: Mfano, armyworm - viwavijeshi, beanfly - nziharage, airfresh - hewasafi.

(iii) Kubuni kwa kutumia vigezo maalumu: Abdomen - fumbato, science - ulimbe, power - ngondo.

(iv) Kuingiza maneno ya Kibantu na ya kilahaja: Hii ndio njia inayopendekezwa na wataalamu wingi. Lahaja husaidia kuziba pengo la msamiati katika kiwango kikubwa. Mfano; newcastle - magwa (Kipemba), leafcurl - mdondo (Kitanzania bara) na weevils - ngozi (Kimtangata). Njia hii ni nzuri na hupokelewa kwa urahisi na watumiaji wake.

Kazi zote hizo zimemsaidia mtafiti kufahamu jinsi lugha ya Kiswahili inavyojitosheleza kimsamiati na pia mtafiti amezifahamu njia mbalimbali za kuunda msamiati.

Pamoja na kuwepo kwa wataalamu wingi walioandika kuhusu lahaja kwa ujumla akiwemo Foucault (1981) na Chambers na Trudgill (1986), vilevile watafiti wingi

wameandika kuhusu lahaja za Kiswahili wakiwemo Sacleux (1909), Stigand (1915), Lambert (1957-1958), Whiteley (1969), Polome (1976), Chiraghdin na Mnyampala (1977), Temu (1980), Maganga (1991), Chum (1994) Kipacha (2003), Massamba (2007) na wingineo. Watafiti wote hao hakuna mtafiti aliyefanya kuhusu tofauti ya mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa lahaja ya Kipemba katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni pamoja na kuandika sababu zinazosababisha mabadiliko hayo. Mtafiti ameamua kufanyia utafiti eneo hilo ili kuziba pengo aliloliona.

2.2.2 Lahaja Mbalimbali za Kiswahili

Masebo na Nyangwine (2004) wameelezea dhima za lahaja ya Kiswahili kama ifuatavyo:

(i) Kukuza lugha: Lugha ya Kiswahili inachukua msamiati kutoka katika lahaja zake na kuziingiza katika Kiswahili.

(ii) Kusanifisha lugha: Kuteuliwa kwa lahaja moja kati ya lahaja nyingi kuwa Kiswahili sanifu, mfano Tanzania, Kiswahili cha lahaja ya Kiunguja Mjini ndicho kilichochaguliwa kiwe Kiswahili sanifu.

(iii) Kuonesha mitindo mbalimbali ya wasemaji na hii hupelekea kutambuliwa kwao mfano; Kipemba - Mpemba, Mombasa - Kimvita, Kikongo - Kingwana.

(iv) Kupamba mazungumzo ya watu mbalimbali, kila lahaja huwa na misemo yake, msamiati na methali japo itakuwa na maana moja.

Kutokana na dhima hizo lahaja ni kipengele kikuu katika lugha hata kama itachaguliwa lahaja moja kuwa rasmi katika mambo yote makuu ya nchi husika lakini bado lahaja zitachukua nafasi yake kati ya wasema lugha moja.

Wataalamu wingi wametafiti lahaja mbalimbali za Kiswahili wakiwemo: Sacleux (1909) anasemekana ni mtaalamu wa mwanzo kuanza kutafiti lahaja hizo. Aligundua kuwa Kiswahili kina lahaja nne kuu kutoka Kusini mpaka Kaskazini, nazo ni Kigunya/Kitikuu, Kiamu, Kimvita na Kiunguja. Naye Stigand (1915), alikuwa ni mtaalamu wa pili lakini amepata idadi kubwa ya lahaja zinazozungumzwa kwenye Kiswahili ukilinganisha na Sacleux, amesema Kiswahili kinachozungumzwa mwambao kina lahaja 16. Baada ya hapo walizuka wataalamu wingi waliochunguza idadi za lahaja hizo ambao hawakutofautiana sana na Stigand.

Masebo na Nyangwine (2004:111) wameorodhesha majina ya wataalamu waliochunguza idadi ya lahaja za Kiswahili kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 2. 1: Idadi za Lahaja ya Kiswahili

Mtaalamu	**Mwaka**	**Idadi**
Chiraghdin	1977	20
Heine	1970	16
Polome	1967	17
Sacleux	1909	04
Stigand	1915	16

Chanzo: Masebo na Nyangwine (2004)

Masebo na Nyangwine (wameshatajwa) wamesema ni dhahiri kuwa wataalamu hao wamepingana katika kutoa idadi ya lahaja za Kiswahili kama ilivyojitokeza hapo juu. Chraghdin (1977) amepata lahaja 20, Dalby (1977) na Polome (1967) wamepata lahaja 17, Heine (1970) na Stigand (1915) wamepata 16 na Sacleux (1915) amepata idadi ya lahaja 4 za Kiswahili. Ni wazi kuwa lahaja za Kiswahili ni kati ya 18 lakini zinaweza zikaongezeka kutokana na ukuwaji wa lugha yenyewe ya Kiswahili. Aina

za lahaja ya lugha ya Kiswahili zimeorodheshwa chini katika jedwali 2.2 kama inavyoonesha hapo chini:

Jedwali Na. 2.2: Aina za Lahaja ya Lugha ya Kiswahili

Na	Lahaja	Eneo
1.	Kiunguja Mjini	Huzungumzwa Unguja hasa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi
2.	Kitumbatu	Huzungumzwa Kaskazini ya Unguja
3.	Kikae (Kimakunduchi)	Huzungumzwa Kusini Unguja
4.	Kipemba	Huzungumzwa katika kisiwa cha Pemba
5.	Kibara	Huzungumzwa katika miji ya Tanzania Bara
6.	Kimvita	Huzungumzwa Mombasa kutoka Malindi (Kusini mwa Mombasa) hadi Gasi (Kusini)
7.	Kivumba	Huzungumzwa katika kisiwa cha Wasini na jimbo la Vanga Mombasa
8.	Kiamu	Huzungumzwa katika kisiwa cha Lamu Kenya
9.	Kipate	Huzungumzwa katika kisiwa cha Pate Kenya
10.	Kishela	Huzungumzwa katika kisiwa cha Shela Kenya
11.	Kisiu	Huzungumzwa katika mji wa Siu
12.	Kitikuu	Ni lahaja ya Rasini na Kaskazini ya Lamu Kenya
13.	Kimtanga'ta	Huzungumzwa mwambao wa mrima katika Tanganyika baina ya Tanga na Pangani
14.	Chifundi	Huzungumzwa Kaskazini ya upwa wa Kenya
15.	Chimiini	Huzungumzwa Mogadishu, Somalia
16.	Kingao	Huzungumzwa Mashariki ya Zaire
17.	Kigwana	Huzungumzwa Zaire na hasa katika jimbo la shaba
18.	Kingozi	Huzungumzwa Kenya

Chanzo**:** Masebo na Nyangwine (2004)

Wataalamu hao wametoa mchango mkubwa sana juu ya idadi ya lahaja za Kiswahili ingawa wataalamu wote hao walikuwa si Waswahili. Walikuwa ni wageni ambao walitafiti sana lahaja za mijini ili watu waweze kuwasiliana kwa urahisi katika mambo ya kibiashara, kidini, kielimu na hata kijamii na hawakuingia ndani kwenye lahaja za vijijini.

Mkude (1993:68) amesema “Ni dhahiri kuwa kila mtu ana namna yake ya kusema lakini upekee wa usemaji wao hauwi wala haupaswi kuwa kikwazo kwa kueleweka na wingine, pia hutambua upekee kwa usemaji wake” aliendelea kufafanua kuwa hii ni kwa sababu katika usemaji wake mtu hulazimika kulingana na jirani zake vyinginevyo hataeleweka. Huo ndio upanuaji wa lahaja kitaaluma. Pia ameonesha msamiati unavyobadilika kulingana na eneo, ametoa mfano wa Kiswahili cha Kenya na Tanzania kama inavyooneshwa kwenye jedwali 2.3 hapo chini:

Jedwali Na. 2.3: Tofauti ya Msamiati kati ya Kenya naTanzania

Mabadiliko	**Kenya**	**Tanzania**
Msamiati	Matatu, kibiriti ngoma	Daladala, changu doa
Matamshi	Ndo, mato	Njo, macho
Muundo	Kibibi ameenda kwa kula	Kibibi ameenda kula
Maumbo	Muongo	Mwongo/muongo

Chanzo: Mkude (1993)

TUKI (2010:49) iliinukuu hotuba ya aliyekuwa wakati huo rais wa pili wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi ya tarehe 13/09/1987. Alinukuliwa akisema “Ijapokua Baraza limepiga hatua kubwa ya kuweza kujivunia, bado kuna kazi kubwa mbele yetu, kwanza ni kuimarisha Kiswahili hapa petu ambapo kunahitaji kutumia hazina zote tulizonazo ndani ya mazingira yetu. Bado hatujafanya utafiti wa kutosha katika lahaja za Kiswahili zinazozungumzwa katika mwambao wa Afrika Mashariki kama lahaja za Kitumbatu, Kimakunduchi, Kipemba (hasa Micheweni).” Hotuba hiyo ilisisimua ari na hasa mstaafu alipogusia Kipemba hasa cha Micheweni, inaaminika kwamba Micheweni bado wanajamii wake wanazungumza lahaja yenye msamiati asilia ya Kipemba.

Mlacha na mwenzake (1995) wameandika kuhusu mradi ulioanzishwa na TUKI unaojuulikana kwa jina la “MRAPA” mwaka 1988, uliokuwa una madhumuni ya kutafuta lahaja za Kiswahili. Moja kati ya mafanikio yake, ulitafiti lahaja za Kiswahili zinavyoweza kujaliza na kuendeleza msamiati wa istilahi yaani (maneno ya kitaalamu au kiufundi) za Kiswahili sanifu. Data zilizokusanywa ni kutoka Zanzibar (Tumbatu na Pemba), kanda ya Kusini Mtwara, Lindi na Kilwa pia kanda ya Mashariki (Bagamoyo, Kisarawe, Mafia na Tanga). Utafiti huu uligundua kwamba vipengele vya Kiswahili sanifu vinaweza kuendelezwa kwa lahaja.

Pia Mwansoko (1992) ameandika kwamba kila mwanaisimu wa Kiswahili anatambua kuwepo kwa hazina kubwa ya msamiati katika lahaja mbalimbali za Kiswahili na msamiati huo unaweza kutumiwa kujaza mapengo ya kimsamiati katika Kiswahili sanifu pamoja na kukiendeleza na kukiimarisha. Alieleza kwa kusema hazina ya msamiati huu wa kilahaja bado haujadhihirishwa kwa yakini na wala haujatumika ipasavyo kukiendeleza Kiswahili sanifu. Hivyo aliamsha hisia kwa mtafiti ya kutaka kuchunguza msamiati wa lugha ya Kipemba ulivyobadilika katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

Nabahany (1995) amesema msamiati bora zaidi ni ule usio mpya hata kidogo kwa hadhira lengwa na uundaji msamiati au istilahi ni mbinu ya kukitanua Kiswahili. Ameonesha njia tofauti ya kuunda msamiati wa Kiswahili na amebuni kwa kutafsiri maana ya viungo vidogovidogo vya maneno vyenye maana kutokana na lahaja za Kiswahili. Kwa mfano:

Ng’andu - dhahabu

Ulimbe - sayansi

Mfumbati - katibu

Pataninga - video

Vilevile Bakhressa (1992) ameelezea tofauti ya msamiati mbalimbali ya kilahaja ikiwemo Kiswahili cha lahaja ya Kitumbatu na Kiunguja Mjini.

Kitumbatu		**Kiunguja Mjini**
Mumucha	-	Fyonza
Mumunya	-	Yeyusha
Mundi	-	Mifupa

Pia Mhina na wenzake (1971) katika makala iliyoharirirwa na Kiimbila waliona tofauti za kiisimu katika Kiswahili. Mfano wa maneno katika lahaja hizi:

Kivumba		**Kiunguja Mjini**
Sungua	-	Chungua
Fuchua	-	Futua
Ngiwa	-	Njiwa

Pia wakatoa tofauti za kiisimu katika Kiswahili cha Chifundi na Kiunguja Mjini kwa kuonesha jinsi ya msamiati unavyotamkwa kulingana na eneo husika kama hapo chini inavyoonesha.

Chifundi		**Kiunguja Mjini**
Mie	-	Miye
Yee	-	Yeye
Swisi	-	Sisi

Kazi hiyo, imedhihirisha kuwa msamiati mbalimbali wa kilahaja unatofautiana sana katika utamkaji kutokana na eneo husika. Kazi hiyo imetimiza ari kwa mtafiti kuikusanya na kuuainisha msamiati wa lahaja ya Kipemba uliyo tofauti katika matumizi yake ya asili katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

Pia Polome (1976) ameeleza uhusiano wa maneno katika lahaja tofauti za Kiswahili, mfano, wingi wa neno **mguu,** Kipemba na Kimombasa wanaita **maguu,** vile vile amebainisha utofauti wa vitamkwa kwa maneno yaliyosawa. Mfano wa Kibajuni na Kisiu wanatumia "**ch"** baada ya "**t",** mfano; cha**ch**u badala ya ta**t**u, m**ch**i kwa m**t**i, pe**ch**e kwa pe**t**e, na hii ni kinyume na Kimvita wao wanatumia "**t"** badala ya "**ch"** mfano bi**ch**i - bi**t**i, m**ch**anga - m**t**anga, ku**ch**eka - ku**t**eka, pia Kipate, Kisiu na Kiamu hawaitamki herufi "**r"** na **"l"** mfano chu**r**a - **chua**, ka**l**e – **kae**, ku**l**eta - **kueta** na vilevile wanatamka "**y"** badala ya "**j"** mfano mo**y**a - mo**j**a, ku**y**a - ku**j**a, ma**y**ani - ma**j**ani na mingineyo. Kazi hii imemsaidia mtafiti kuona jinsi ya utamkaji wa msamiati mbalimbali katika lahaja za Kiswahili ambapo zimemshawishi mtafiti kuchunguza mabadiliko ya matumizi katika lahaja ya Kipemba.

Naye Haji (2006) amepiga hatua kubwa kwa kuyaandika maneno ya Kitumbatu na kuyatolea maana katika Kiswahili sanifu, kwa mfano; buku - kibutu, buchari - jisu, bukuya - nyofoa, cha - ncha, chachurika - changamka, chavuga - chafua, dosa - gusa.

Pia matokeo ya utafiti wa Ali (2007) aliyechunguza athari za usasa katika lahaja ya Kitumbatu asilia yaliibua fikra mpya katika utafiti huu. Ali alitaka kujua kwa kiasi gani lahaja ya Kitumbatu (iliyopo Kaskazini Unguja), ilivyoathiriwa na usasa kwani msamiati mwingi wa asili ya Kitumbatu hautumiki hivi sasa. Vilevile aligundua

kuwepo lahaja ndogondogo ndani ya lahaja kuu, ambazo hulingana sana kimsamiati, kimuundo, kwa wasemaji wake ingawa hutofautiana katika lafudhi.

Kipacha (keshatajwa) amesema Kimakunduchi huzungumzwa sehemu za Kusini Mashariki mwa visiwa vya Uzi, Bwejuu na baadhi ya vijiji vya Jambiani upande wa pwani wa Kaskazini Makunduchi, upande wa Magharibi katika sehemu za Kizimkazi na Muyuni. Pia Stigand (keshatajwa), amesema Kimakunduchi na Kitumbatu ni lahaja zenye uhusiano na zina mfanano mkubwa hadi kufikia kuitwa lahaja moja ya Kihadimu. Kihadimu ni lugha inayohusisha lahaja ya Mashariki na Kusini (Kimakunduchi) na ile ya Kaskazini ya Unguja (Kitumbatu). Pia hakutofautiana sana na Chiraghdin na Mnyampala (1977) wao wameeleza kuwa Kihadimu (Kimakunduchi na Kikae), ni lahaja ya Kusini na Mashariki mwa Unguja. Walisema lahaja hiyo ina maneno mingi zaidi ya Kiswahili cha kilahaja na machache sana kutoka lugha nyingine za kigeni, kama lahaja ya Kipemba na lahaja nyingine za Kiswahili.

Juma (2006) aligundua kuwepo kwa lahaja ndogondogo zinazotokana na lahaja kuu ya Kimakunduchi ambazo zina mfanano wa msamiati na maumbo yake katika lahaja za Kijambiani, Kipaje na Kibwejuu. Mfano wa maneno yenye mfanano ni kama kanamkaza - anampenda, mnafana - mnapendeza. Ingawa vilahaja hivyo baadhi ya wakati hutofautiana katika maumbo ya maneno mfano wa neno "**evu",** wote wanatumia mzizi **"evu"** katika vitenzi vyao, mfano wa maneno **"aliolewa"** na **"tuliapa".**

Kimakunduchi: k**evu**kaolegwa, tw**evu**tulapa

Kibwejuu: k**evu**kaolegwa, k**evu**tulapa

Kipaje: **evu**gakaolegwa, **evu**gatulapa

Kijambiani: kaolegwa, tulapa. (Hawa hawatumii evu/kevu).

Vilevile utafiti wa Juma (2011) ambaye alilinganisha msamiati wa Kimakunduchi, Kibwejuu, Kimtende na Kizimkazi, aligundua kuwa Kibwejuu na Kimtende kinatokana na lahaja kuu ya Kimakunduchi na Kizimkazi si miongoni mwa lahaja za Kimakunduchi kwani Kizimkazi kimeathiriwa sana na Kiunguja Mjini.

Pia Chum (keshatajwa), ameukusanya msamiati pekee wa Kikae (Kimakunduchi) mfano; adi - bin, agaa - chukua. Amegundua sehemu kubwa ya Kusini Unguja hutumia Kikae kama vile Pete, Jozani, Paje, Jambiani, Muongoni, Muyuni, Kizimkazi, Mtende na Makunduchi yenyewe ambayo ndio makao makuu ya lahaja ya Kikae na Kaskazini hutumia Kitumbatu. Kutokana na fikira za watafiti hao wamemtia ari mtafiti kuchunguza lahaja za Kipemba.

2.2.3 Lahaja ya Kipemba

Wataalamu wingi waliotafiti lahaja za Kipemba wamehitilafiana katika kutoa idadi ya lahaja hizo. Mfano; Sacleux (1909) alipata lahaja nne (4), Batibo (1982) alipata lahaja mbili (2) wakati Temu (1980) yeye aligundua Kipemba kimoja (1) tu sawa na Hamad (2011), Polome (1979) lahaja tatu (3) na Nurse (1982) mbili (2).

Khamis (1984) ameelezea wataalamu tofauti waliochunguza idadi ya lahaja za Kipemba na akaonesha idadi tofauti ambazo wanalughawia wamepata katika utafiti wao. Idadi ya lahaja hizo ni kama zinavyooneshwa na Jedwali 2.4 hapo chini:

Jedwali Na. 2.4: Idadi ya Lahaja ya Kipemba

Mtaalamu	**Mwaka**	**Idadi**	**Makundi ya Lahaja**
Sacleux	1909	04	Kivitongoji, Kichakechake, Kimsuka na Kipemba Mjini.
Polome	1976	03	Kipemba cha Kaskazini (Konde, Tumbe, Micheweni), Kipemba cha Kati, (Kiwani, Matele, Kiuyu na Kambini) na Kipemba cha Kusini
Temu	1980	01	Kipemba kimoja tu.
Batibo	1982	02	Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.
Nurse	1982	02	Kipemba sanifu na ambacho sio sanifu.
Hamad	2011	01	kipemba kimoja tu

Chanzo**:** Khamis (1984)

Naye Chiraghdin na Mnyampala (1977) wamesema kuwa lahaja za lugha ya Kiswahili zipo ambazo zinaingiliana katika matumizi ya baadhi ya msamiati. Wakaeleza kuwa Kimtang'ata kinachanganya maneno ya Kipemba na Kitumbatu. Pia akasema upo msamiati ambao unatumika katika lahaja ya Kimvita na Kivumba lakini pia unatumika katika Kipemba. Mfano wa msamiati huo ni;

Amba - labda

Ganga - siri

Uya - rudi

Kibunju - Kijana mdogo

Pia maneno hayohayo yameelezwa na Whiteley (1956) kwamba Kipemba na Kitumbatu kimechukua msamiati mwingi kutoka Kimtang'ata. Yeye akatoa mifano ya msamiati ufuatayo: Kwani? - Kwanini

Tuuye - Tuondoke

Afanya/efanya - Kafanya

Hata Khatib (2010) alizungumzia historia na maendeleo ya Kiswahili Zanzibar, kupitia lahaja kuu nne za Zanzibar: Kikae (Kimakunduchi), Kitumbatu, Kipemba na Kiunguja Mjini. Amesema Kipemba kinatofautiana katika maongezi na lahaja nyingine za Zanzibar. Alifafanua kuwa si lahaja zote za Pemba zinakubaliana, kila ukisogea ndani zaidi ndipo unapokuta lahaja safi kabisa, isiyo na athari za mji wala za kigeni. TUKI (2010) nao wameelezea kuhusu lahaja kuu nne (4) ambazo ni Kiunguja (husemwa Mjini), Kihadimu (husemwa katikati ya Kusini na Magharibi), Kitumbatu (husemwa kisiwani Tumbatu na sehemu za Kaskazini ya Unguja) na Kipemba (huzungumzwa kisiwani Pemba). TUKI walisema pia kuwa wenyeji wingi wa Zanzibar wametoka Mrima na kwamba baada ya Uislamu kuingia Zanzibar na kuzagaa na Wabantu wingi kusilimishwa, mabinti wa Kibantu wakaolewa na Waarabu na Washirazi, na hapo Kiswahili ambacho ni lugha mpya ikazaliwa.

Kutokana na mawazo hayo ni dhahiri kusema kuwa wataalamu wingi wa Kiswahili wameungana kusema kuwa Kiswahili cha lahaja ya Kipemba kina lahaja nyingi ingawa mpaka sasa imeshindikana kutolewa mawazo ya pamoja ya idadi hasa za lahaja za Kipemba. Hata hivyo utafiti mkubwa unaonesha umefanywa na wageni ambao si Waswahili. Mapitio haya yalimsaidia mtafiti kupata mwamko wa kuelewa mawazo tofauti ya wataalamu hao.

Maganga (1991) amelinganisha fonolojia katika lahaja nne za Kisiwani Zanzibar ambazo ni lahaja ya Kiunguja Mjini, Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba. Aligundua kuweko kwa mfanano na mtofautiano kati ya lahaja hizo katika fonolojia, mofolojia na msamiati; mfano mzuri alitoa tofauti za nyakati katika wakati uliopo.

Aligundua utofauti katika vitamkwa na mofimu katika msamiati, akaonesha Kiunguja Mjini kinavyotofautiana na Kimakunduchi katika nyakati (njeo). Mfano; wakati uliopita.

Kiunguja	**Kimakunduchi**
Niliona	Nyono
Niliuza	Nyuzu
Nilisuka	Nsuku

Vilevile ameonesha tofauti baina ya lahaja za Zanzibar katika baadhi ya mchakato yake ya kifonologia au kimofolojia. Mfano wa tofauti ya vitamkwa vya mofimu katika msamiati unavyodhihirishwa na jedwali 2.5 hapa chini:

Jedwali Na. 2.5: Tofauti ya Vitamkwa vya Mofimu katika Msamiati

Kiswahili sanifu	**Kipemba**	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
Mti	Nti	Mjiti	Ujiti
Sisi	Siye	Suye	Suwe
Mimi	Miye	Miye	Miye

Chanzo: Maganga (1991)

Pia Khamis (keshatajwa) amechunguza lahaja ya Kipemba Mjini na kugundua kuwa wazungumzaji wa Mjini Pemba wanatumia **m** au **me** mwazoni mwa neno lakini wa vijijini asilimia 6 tu ndio wanotumia **m** au **me** na hutumia **n** au **na**. Kwa mfano;

Mjini - **M**kate ni**me**utia **m**kobani.

Vijijini - **N**kate n**na**utiya **n**kobani.

Mjini - Ni**mem**laza kitandani **m**toto wako.

Vijijini - **N**na**n**laza kitandani **n**totowo

Katika uchunguzi wake, amechangia sana kuibua fikra za utafiti huu, kwa kuonesha tofauti ya lafudhi ambayo inahusu kuyatamka maneno. Yeye kaidhihirishia jamii kwamba tofauti ya lafudhi ni jambo muhimu sana, lisiloweza kuepukika katika lugha.

Faki (2011) kaonesha mitindo mbalimbali ya utamkaji wa maneno katika lahaja ya Kipemba, kwa mfano; Wizi - waizi, kaja - kankuja, wawili - waili, kweya - panda.

Pia akatoa mifano tofauti juu ya utamkaji wa mnyambuliko wa maneno kama:

Niletea samaki - niletee samaki,

Niuliza swalilo - liulize swali lako.

Pia akaonesha muunganisho wa maneno yanayounganisha nomino na kivumishi katika Kipemba. Mfano; Watu wake - watuwe, vitu vyako - vituvyo.

Pia akasema Wapemba wanatumia **"e"** kuonesha kitendo kilichopita mfano:

Kipemba: **E**kuja lakini henikuta.

K/Fasaha: **A**likuja lakini hakunikuta.

Kipemba: **E**kufa bado yundogo.

K/Fasaha: **A**likufa bado mdogo.

Pia **e** hiyohiyo hutumika katika kihisishi, kwa mfano:

Kipemba: **E**! mpisha vyangu hapa.

K/Fasaha: **We!** Nipishe mimi hapo.

Kipemba: **E**! mwambie endevye.

K/Fasaha: **We!** Mwambie ende zake

Vilevile akaonesha matumizi ya neno "**hi"** inavyotumika Upembani; mfano:

Kipemba: **Hi**ntizama kwa uchungu.

K/Fasaha: **Nili**mtazama kwa hasira.

Kipemba: **Hi**zipata tu najenga.

K/Fasaha: **Nik**izipata tu najenga.

Vilevile Mshindo (1988) alionesha matumizi mbalimbali ya mofimu "**ka**" katika Kiswahili cha Kipemba, huyu alibainisha kuwa mofimu **"ka"** hutumika katika msamiati ya Kipemba ikiwa na maana tofauti, kwa mfano:

Huamka ni**ka**lima.	**ka** - Inaelezea vitendo.
Nenda **ka**mwambie aje upesi.	**ka** - kitendo cha amri
Kampona? **Ka**shauza?	**Ka** - kuuliza (swali)

Kipacha (2007) ameandika orodha ya leksimu tofauti za msamiati wa lahaja za Kiswahili ikiwemo Kipemba na kuitolea tafsiri katika lugha sanifu. Kwa mfano, amba - labda, bereuza - pindua, bwaga - angusha.

Whiteley (1958) ameandika maneno ya Kipemba na baadaye kuyawekea fasili yake kama inavyoonesha katika jedwali 2.6 lililopo hapo chini.

Jedwali Na. 2.6: Maneno ya Kipemba na Kiswahili Fasaha

Kipemba	**Kiswahili Fasaha**
Kijio	Chakula cha mchana
Mbaumbi	Mlo mkubwa
Vyaa	Zaa
Nsongo	Foleni
Kombefu	Mabega
Mwiku	Uporo

Chanzo: Whiteley (1958)

Said (2011) amezungumzia viangami katika Kipemba, kuwa viangami ni vipashio vinavyoungwa na neno na vilevile ni neno linalokatwa Upembani. Akaainisha mifano ya viangami mbalimbali vinavyotumika katika lahaja ya Kipemba mfano:

Kipemba: **Yu wa**?

K/Fasaha: Yu**ko** wa**pi**?

Kipemba: Si fanyi **ta** unipige.

K/Fasaha: Sifanyi **hata** ukinipiga.

Kipemba: Takuja hukohuko nyumbani**ko.**

K/Fasaha: Nitakuja hukohuko nyumbani kwa**ko**.

Pia mtafiti aliupitia utafiti wa Gora (2011) uliotafiti mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo. Moja ya lahaja inayotumika kwenye nyimbo hizo ni lahaja ya Kipemba na akaigiza nyimbo nyingi zilizotumia msamiati wa lahaja hiyo mfano; nyimbo ya uganga wa peuo ya wavyele ambapo inatumia msamiati mwingi wa Kipemba. Ndani ya nyimbo hiyo yapo maneno ya lahaja hiyo. Kwa mfano, *nombe* - niombe, *wavyele* - wazazi, *mwanangwa* - mtoto wa watu, *dade* - dada, *yasaliako* - yanakobakia na mingineyo.

Vilevile Hamad (2011) alionesha kwa kiasi kikubwa jinsi ya nyakati zinavyozungumzwa katika lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu, lakini lugha aliyoitumia ni Kiingereza na watumiaji wingi wa Kiswahili kukosa kuelewa lugha hiyo. Hivyo utafiti huu kwa vile ni wa Kiswahili, unafanywa na Mswahili, basi utaandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuwarahisishia wasomaji kufahamu kilichokusudiwa kwa urahisi kabisa.

Aidha wapo watafiti waliofanya utafiti kuhusu lahaja ya Kipemba akiwemo Faki (2011), aliyetafiti matumizi ya mofimu **“e”, “ha”** na **“he”** katika utamkaji wa lahaja ya Kipemba, Hamad (2011) aliyeshughulikia nyakati zinavyozungumzwa katika Kiswahili sanifu na Kipemba, Khamis (1984) alitoa tofauti ya matamshi kati ya Kipemba cha mjini na cha shamba na Mshindo (1988) ambaye alitafiti mofimu **“ka”** katika lahaja ya Kipemba. Hivyo mtafiti kaona pengo katika uwanja huu ndipo kwa makusudi akaamua kuchunguza utofauti wa mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba katika miktadha ya harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

2.3 Pengo la Utafiti

Lahaja ya Kipemba ni moja wapo kati ya maeneo yaliyofanyiwa sana utafiti. Licha ya kuwa lahaja hii imeanza kutafitiwa miaka ya zamani toka 1909 na kuendelea na utafiti katika maeneo tofauti, tafiti hizo hazijatosheleza kwani bado kuna maeneo mingi yanayohitaji kufanyiwa utafiti. Baada ya kutalii kazi za wataalamu mbalimbali waliozungumzia lugha ya Kiswahili, lahaja za Kiswahili ikiwemo ya Kipemba, mtafiti amegundua kuwa hadi sasa hakuna andiko lolote lililoandikwa kuhusu “Kiwango cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati wa Lahaja ya Kipemba”.

Hivyo utafiti huu umekusudia kuziba pengo kwenye eneo hilo. Utafiti utajihusisha na muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni na wataalamu watakaofuatia wanaweza kuendeleza katika muktadha wa shuleni, ofisini, sokoni, mazungumzoni na miktadha mingineyo. Utafiti huu umebainisha vipengele muhimu ambavyo ni kuuainisha msamiati wa Kipemba ambao umebadilika matumizi yake katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni, kutathmini tofauti ya kiasi cha

mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia kwa kila muktadha husika na lengo la mwisho ni kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo.

2.4 Mkabala wa Kinadharia

Verschurch (2005) ameeleza kwamba nadharia ni njia ambazo husaidia katika utoaji maoni, mawazo ambayo yatamfanya mtafiti kupata maoni ya kazi yake. Sengo (2009) amesema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu wa mtu au watu (jamii) pahala fulani, wakati fulani na ni muongozo wa kufuata wakati wa kuchambua kazi za utafiti. Utafiti huu umeongozwa na nadharia zifuatazo: “Nadharia ya Mwenendo na Mabadiliko”, “Nadharia ya Ubadilikaji” na “Nadharia Kidhi ya Mawasiliano”.

2.4.1 Nadharia ya Mwenendo na Mabadiliko

Nadharia hii ya Foucault (1981) imeeleza kuwa lugha hukua na kubadilika ingawa si lazima mabadiliko hayo yawe sambamba na mabadiliko katika jamii yote, akashadidia kwa kusema, ujuzi wa lugha tuliyonayo hutuwezesha kutoa na kuelewa msamiati na sentensi mpya kila siku kama kanuni za msingi za lugha yeyote zitafuatwa. Hivyo lugha zimefungamana sana na mfumo, mwenendo na mabadiliko ya maisha ya binaadamu. Pia Mhina na wenzake (1977) wamesema kitu chenye uhai lazima kibadilike, akatoa mfano wa mtoto hukua kupitia hatua nne; utoto, ujana, makamo na uzee. Mfano huo akauhaulisha na lugha, akasema kama lugha ipo hai ni lazima ikue. Lugha hubadilikabadilika kutegemea mazingira ya pale inapotumiwa. Mabadiliko hayo hutokea katika sauti, miundo na mpangilio wa maneno na maana.

Mabadiliko makubwa hutokea kwenye maneno na maana. Nadharia hii imetumika kuuongoza utafiti kufikia lengo lake la kwanza ambalo ni kuuainisha msamiati wa Kipemba katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini kwa kuonesha mabadiliko hayo yalivyo kwa sasa katika msamiati huo.

2.4.2 Nadharia ya Ubadilikaji

Massamba (2007) amemnukuu Darwin (1838) alivyoielezea nadharia ya ubadilikaji wa lugha ambayo msingi wake kwamba mabadiliko ya lugha hutokana na harakati za ushirikiano, masikilizano na maingiliano ya binaadamu na mazingira yake. Pia anaitakidi kuwa katika maisha ya binaadamu vitu vyote hubadilika, ikiwemo lugha, lugha hubadilika kutoka hatua moja hadi nyingine, kadri wakati unavyobadilika. Mabadiliko hayo hutokea kidogokidogo kiasi ambacho watumizi wa lugha husika hawawezi kugundua kwa uharaka mabadiliko yale. Mzee wa miaka sabiini hawezi kuwa na matumizi yaliyosawa na vijana licha ya kuwa wanatumia lugha moja na wanaelewana vizuri.

Nadharia hii iliuongoza utafiti kufikia lengo lake la pili ambalo ni kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia ili kujua ni muktadha upi umebadika zaidi na upi haujabadilika katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni kwa kuorodhesha msamiati wa muktadha husika na kulinganisha kiasilimia kiwango cha mabadiliko hayo. Kwani nadharia hii imeeleza kuwa mabadiliko hayo hayagunduliki kwa haraka kiwango cha ubadilikaji wake. Hivyo nadharia hii imetumika kutathmini kiwango halisi cha ubadilikaji wa msamiati huo kwa kuulinganisha kiasilimia katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.

2.4.3 Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM)

Hii ni nadharia iliyoanzishwa na Giles, (1973), ambayo ilijaribu kutafuta sababu za kuwepo kwa mabadiliko ya wazungumzaji katika mtindo wa matamshi na msamiati mpya wakati wa mawasiliano ya kijamii. NKM imesema kuwa binaadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna fulani ya matamshi ya lugha na msamiati mipya kutoka kwa msikilizaji wake ili tu aweze kukidhi haja ya mawasiliano. Hufanya hivyo ama kwa kujua au kutokujua, kwa kufikiria au bila kufikiria na huiga msamiati au vipengele vyingine vya lugha kwa mtu anaezungumza naye kwa lengo la kukubalika katika jamii hiyo. Giles amefafanua kuwa sababu kuu ya kubadili mtindo wa matamshi na msamiati ni kuonesha makubaliano na uhusiano kwa watu wingine. Hali hii huwafanya watu wingi kujihisi kuwa wanahusiana. Nadharia hii imeuongoza utafiti kufikia lengo maalumu la tatu ambalo ni kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba.

2.5 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeonesha kazi tangulizi za wataalamu tofauti ambazo mtafiti alizipitia zinazohusiana na lugha ya Kiswahili, lahaja mbalimbali za Kiswahili pamoja na lahaja ya Kipemba. Aidha, pengo la utafiti lilioneshwa. Mwisho, sura hii imeonesha mkabala wa kinadharia ambao uliuongoza utafiti huu na imefafanuliwa na kubainishwa sababu za kutumia nadharia hizo katika kulifikia lengo kuu la utafiti kama ilivyotarajiwa.

SURA YA TATU

3.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha njia na mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu, mipaka ya utafiti na uteuzi wa watafitiwa. Vilevile ikafafanua mbinu za usampulishaji wa watafitiwa, utaratibu wa ukusanyaji wa data. Mwisho ikaelezea mbinu zilizotumika katika kuchambua na kuchanganua data na sura hii ikahitimisha kwa muhtasari wa sura.

3.2 Mbinu za Kukusanyia Data

Kothari (1985) amesema mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Utafiti huu ulitumia njia ya hojaji, usaili na maelezo ili kupata data za utafiti kutoka kwa watafitiwa.

3.2.1 Njia ya Hojaji

Denskombo (2005) ameielezea kuwa hii ni njia ya utafiti ambayo mtafiti huandaa maswali yanayoongoza kutoa taarifa ya utafiti wake kwa kuyaandika na mtafitiwa hutakiwa ajibu kwa maandishi, pia mtafiti hupata wahojiwa wingi kwa muda mfupi. Mtafiti ametumia njia hii kwa kuandaa maswali ya hojaji yenye maswali mchanganyiko yaliyolenga malengo ya utafiti. Njia hii iliwahusisha zaidi watafitiwa wanaojua kusoma na kuandika ambao walikuwa 32, wazee 14 na vijana 18. Mtafiti ametumia watu wanaojua kusoma na kuandika kwa sababu wanaweza kutoa maelezo yao vizuri na yenye kufahamika na pia wanaweza kueleza mingi kwa vile wanapojaza hojaji wanakuwa wapo faragha. Ingawa njia hii ilipata changamoto ya

maswali ya hojaji kuathiriwa na baadhi ya wahojiwa kwa kutokuwa na haiba (muonekano ama mvuto wa wasifu wa mtu kuwa na utayari katika jambo), imani na mitizamo tofauti kwa wahojiwa. Matatizo haya mtafiti ameyatatua kwa kutafuta siku ambayo watafitiwa walikutwa wapo kwenye haiba.

3.2.2 Njia ya Usaili

Hii ni njia ambayo inamuwezesha mtafiti kukutana ana kwa ana na watafitiwa na kupata majibu ya haraka. Pia njia hii humsaidia sana mtafiti ikiwa swali litashindikana kujibika huweza kubadilisha swali jingine hapohapo lenye maudhui sawa na swali lile. Aghalabu huwa maswali madogo madogo/mafupi mafupi, Seidman (1991). Mbinu hii ilitumika kwa watafitiwa 26, watafitiwa 13 wa kundi la vijana na 13 wa kundi la wazee. Mtafiti ametumia mbinu hii katika idadi hiyo kwa sababu ameona atapata data nyingi kwa vile atakutana nao ana kwa ana na walengwa. Matatizo yaliyomkabili mtafiti kwa kutumia njia ya usaili, wingine kushindwa kutoa maelezo ya moja kwa moja kutokana na tatizo la kutokuweza kujieleza vizuri. Mtafiti alifanya njia mbadala ya maelezo kwa watafitiwa ambao hawawezi kujieleza vizuri.

3.2.3 Njia ya Maelezo

Khamis na wenzake (1990) wamesema maelezo ni taarifa zitolewazo kwa njia ya mdomo (masimulizi), ni maelezo yanayotoka moja kwa moja katika kinywa cha mzungumzaji kwenda kwa msikilizaji. Njia hii iliwahusisha watafitiwa 31, wazee 15 na vijana 16. Kundi hili wingi wao hawawezi kujieleza vizuri na baadhi hawajui kusoma wala kuandika.

3.3 Mipaka ya Utafiti

Mtafiti ameushughulikia msamiati wa lahaja ya Kipemba tu katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni. Vilevile utafiti huu umefanyika katika vijiji vinne, kimoja kila wilaya iliyopo kisiwani Pemba. Maeneo yaliyohusishwa ni:

Wilaya ya Micheweni - Kijiji cha Kiuyu

Wilaya ya Wete - Kijiji cha Kojani

Wilaya ya Mkoani - Kijiji cha Kiwani Nanguji

Wilaya ya Chakechake - Kijiji cha M/Malofa

3.4 Mbinu za Usampulishaji wa Watafitiwa

Upatikanaji wa vijiji, ulitumia njia aliyoipendekeza Ruane (2005) ya bahati nasibu. Njia hii kaifafanua kuwa ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo kila mshiriki katika kundi lengwa ana fursa sawa ya kuchaguliwa na kushiriki katika utafiti. Mtafiti aliyaorodhesha majina matano matano ya vijiji kwa kila wilaya iliyopo Pemba na baadaye kumtafuta mtoto achague karatasi yenye jina la kijiji kimoja wapo kutoka kila kundi. Mtafiti amevipendekeza vijiji vya Kiwani Nanguji, Kojani na Kiuyu kwa sababu wanavijiji wake wanaonekana kuwa bado wanatumia lahaja ya Kipemba cha asili na hakina mchanganyiko wa wageni.

Vilevile amekipendekeza kijiji cha Mkungumalofa kwa sababu kipo Mjini Chakechake na kwa sasa inaaminika kuwa Wilaya hiyo ndiyo kitovu cha kisiwa cha Pemba kwa kuwepo huduma zote zinazohitajika kuitwa mji. Aghalabu kwenye miji mikubwa ya Mikoa au Wilaya katika nchi huwa na mchanganyiko wa watu na lugha ama lahaja zao. Lugha za asili za miji hiyo hudhoofika.

Kwa upande wa wahojiwa, makundi yote mawili ya wazee na vijana yalipatikana kwa njia ya bahati nasibu. Kothari (1985) amesema ni vyema mtafiti kutumia njia ya nasibu ili aweze kutoa nafasi sawa na kuepuka ubinafsi na upendeleo. Kundi la vijana lilihusisha watafitiwa 49 na kundi la wazee lilihusisha watafitiwa 40. Mtafiti amelichagua kundi la vijana kwani ndio washiriki wakuu katika shughuli za kijamii ikiwemo harusi pia ndio nguvu kazi kilimoni na uvuvini. Mtafiti alihesabu nyumba nne na ya tano ndimo alimopata mtafitiwa. Nalo kundi la wazee lilichaguliwa kwa sababu ni watumiaji wazoefu wa msamiati wa lahaja yao asilia ya Kipemba na huwa hawana mchanganyiko sana na jamii nyingine. Mtafiti alipita kwenye vijiji lengwa, na kufanikiwa kuwahoji baadhi ya wazee waliokuwa wamekaa kwenye maskani. Jedwali lifuatalo linawasilisha watafitiwa hao kwa muhtasari.

Jedwali Na. 3.1: Idadi na Matabaka ya Watafitiwa

WILAYA	**MKOANI**		**CHAKE**	**WETE**			**M/WENI**		**JUMLA KUU**		
VIJIJI	**K/NANGUJI**		**M/MALOFA**	**KOJANI**			**KIUYU**				
WATAFITIWA	**WK**	**WM**	**WK**	**WM**	**WK**	**WM**	**WK**	**WM**	**WK**	**WM**	**JUML**
VIJANA	07	06	06	06	06	06	05	07	**24**	**25**	**49**
WAZEE	04	06	03	06	04	06	05	06	**16**	**24**	**40**
JUMLA KUU	11	12	09	12	10	12	10	13	**40**	**49**	**89**

Chanzo: Mtafiti (2014)

3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji wa Data

Data zimekusanywa kulingana na utaratibu uliopangwa na mtafiti. Mtafiti alifika katika vijiji alivyovilenga na kujitambulisha kwa wakuu wa vijiji hivyo ambao ni

Masheha. Masheha hao walitoa ushirikiano mzuri katika kuwapata watafitiwa wa makundi yote ya wazee na vijana. Kwanza mtafiti alianza utafiti wake katika Wilaya ya Wete, kijiji cha Kojani kwa kuwahoji na kuwasaili vijana, baadaye akaendelea na wazee. Halikadhalika mpangilio huo huo uliendelea katika Wilaya ya Micheweni kwa kijiji cha Micheweni kisha alielekea Wilaya ya Mkoani, katika kijiji cha Kiwani Nanguji na mwisho mtafiti alimalizia katika Wilaya ya Chakechake kwa wanakijiji wa M/Malofa na hapo mtafiti akawa amekamilisha utaratibu wake wote aliojipangia wa ukusanyaji wa data.

3.6 Mbinu za Kuchambua na Kuchanganua Data

Kwa mujibu wa Williman (2011) amesema data huchanganuliwa katika mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala usio wa kiidadi. Mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo hutumia nambari kurikodi taarifa na huchanganuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu. Nae Enon (1998) ameeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Kwa kuzingatia umuhimu wa kila mkabala, utafiti huu ulitumia mikabala yote miwili. Aidha, mtafiti ametumia mkabala wa kiidadi na wa kimaelezo katika lengo la kwanza kwa kuainisha msamiati wa Kipemba ambao umebadilika matumizi yake katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni. Pia ulitumia mkabala wa kiidadi kwa lengo la pili ambalo ni kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kwa muktadha husika. Vilevile ametumia mkabala usio wa kiidadi (maelezo) kwa lengo la tatu ambalo ni kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba. Pia mtafiti ametumia mbinu iliyopendekezwa na

Chambers na Trudgill (1986), katika kuchanganua data kwa wanaisimu (wanalughawia) kutumia mbinu ya lahaja kijiografia. Mbinu hii imezingatia uhalisia wa kukusanya data huku ikizingatia makundi ya kijamii na tofauti ya maeneo wanayoishi watafitiwa. Wanalughawia hupata data za ukweli, pia inazingatia aina ya maswali ya kuuliza kulingana na jamii husika kwani amebainisha kuwa huwezi kuuliza maswali ya mjini yakawa sawa na vijijini kutokana na tofauti yao ya uzungumzaji uliyosababishwa na mazingira.

3.7 Muhtasari wa Sura

Sura hii imefafanua namna ya utafiti ulivyofanyika. Kipengele cha kwanza ambacho ni mbinu za kukusanyia data alizotumia mtafiti zimeelezewa, mipaka ya utafiti, mbinu za usampulishaji wa watafitiwa. Pia utaratibu mzima wa ukusanyaji wa data ulivyokuwa na mwisho imeelezea mbinu za kuchambua na kuchanganua data.

SURA YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii imezingatia uwasilishaji na uchambuzi wa data kuhusu kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba. Msamiati huo ulikusanywa kwa muda wa miezi miwili kuanzia tarehe 15/4/2014 mpaka tarehe 12/6/2014. Jumla ya msamiati 57 ya lahaja ya Kipemba ambayo imebadilika katika matumizi yake imekusanywa kati ya msamiati 60 ya idadi iliyotarajiwa sawa na 95% ya msamiati wote. Mtafiti alilenga kupata msamiati 15 kwa kila muktadha lakini alifanikiwa kukusanya msamiati 19 kati ya 15 aliyoilenga sawa na 126.67% kwa upande wa msamiati wa harusini. Pia alikusanya msamiati 12 wa msibani kati ya 15 sawa na 80%, msamiati 13 wa uvuvini kati ya 15 sawa na 86.67% halikadhalika msamiati 12 kati ya 15 unaotumika kilimoni sawa na 86.67%. Data zote zimepatikana kwa kutumia njia ya hojaji, usaili na maelezo na zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa kina katika sura hii.

Data hizo zimepatikana kutoka kwa watafitiwa wa makundi ya wazee na vijana. Sura hii imeanza kwa kuwasilisha data na kumalizia kwa uchambuzi wa data uliyozingatia malengo maalumu ya utafiti huu ambayo yalilenga kuuainisha msamiati wa Kipemba na baadaye kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya msamiati huo katika miktadha ya harusini, uvuvini, msibani na kilimoni na hatimaye kuchambua mambo yaliyosababisha mabadiliko hayo. Uchambuzi na uchanganuzi wa data umewasilishwa kwa kuzingatia malengo maalumu kama inavyoonesha hapo chini:

4.2 Uainishaji wa Msamiati

Lengo maalumu la kwanza, ni kuuainisha msamiati wa harusini, msibani, uvuvini na wa kilimoni wenye asili ya Kipemba ambao umebadilika katika matumizi yake. Lengo hilo liliongozwa na swali la kwanza lililouliza kuwa; Ni msamiati upi wa Kipemba ambao umebadilika matumizi yake katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni? Katika kufikia lengo nadharia ya mwenendo na mabadiliko ya Foucault (1981) imetumika kuongoza kufikia lengo lake kama ilivyofafanuliwa nadharia hiyo katika uk. (30).

4.2.1 Msamiati wa Harusini

TUKI (1981) imefasili dhana ya harusi kuwa ni ndoa, nikai, uozi, akidi. Bakhressa (1992) amefasili harusi ni ndoa, nikakha au sherehe ya ndoa. Tunaweza kusema harusi ni tendo la makubaliano kati ya mwanamke na mwanamme walioridhiana kufunga ndoa kwa hali na mali kisheria. Pemba neno hili wanalinyambua, harusi (nomino), harusika (kitenzi) ni kuwa na harakati za harusi. Wahusika wakuu wa harusi ni mwanamke anaitwa bi harusi na mwanamme anaitwa bwana harusi. Mtafiti ameugawa msamiati wa harusini katika mikabala mitatu kimatumizi yaani kabla, wakati na baada ya harusi kama ifuatavyo:

4.2.1.1 Msamiati Unaotumika Kabla ya Harusi

Msamiati huu hutumika wakati inapoanza tetesi za posa tu. Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, usaili na maelezo kupitia katika makundi ya vijana na wazee kwa kutumia zana zao za maswali kwa kundi husika. Matokeo yanaoneshwa kwenye jedwali 4.1 hapo chini.

Jedwali Na. 4.1: Msamiati Unaotumika Kabla ya Harusi

	Msamiati							Mfano wa sentensi
	Msamiati wa Awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Kisw/Sanifu**	
1.	Chunguuwa	53	60%	Chunguuza	36	40%	Chunguza	**Zamani:** Ntu muume *tushanchunguuwa* tabiaze ni nzuri **Mabadiliko:** Ntu muume *tushanchunguuza* tabiaze ni nzuri **Kisw/Sanifu:** Mwanamme *tumemchunguza* tabia zake ni nzuri
2.	Dunga	48	54%	Tunga	41	46%	Tunga	**Zamani:** Leo ntaka *dunga* shanga za biharusi. **Mabadiliko:** Leo ntaka *tunga* shanga za biharusi. **Kisw/Sanifu:** Leo nataka *kutunga* shanga za biharusi.
3.	Kifunga-nlyango	32	36%	Kifunganlango/	57	64%	Kifunga-mlango	**Zamani:** Wanlipa laki nzima ya kifunguanlyango. **Mabadiliko:** Wanlipa laki nzima ya *Kifunguamlango /kifunguanlango*. **Kisw/Sanifu:** Wameshalipa laki nzima ya *kifunguamlango*.
4.	Kukata-mahari	47	53%	Kudai- mahari	42	47%	Kudai-mahari	**Zamani:** Babeye *keshakata mahari* ya Asha. **Mabadiliko:** Babeye *keshadai mahari* ya Asha. **Kisw/Sanifu:** Baba yake *ameshadai mahari* ya Asha.
5.	Mposhi	41	46%	Mposi/	48	54%	Nshenga	**Zamani:** *Mposhiwo* kila siku aja na kesi. **Mabadiliko:** *Mposiwo* kila siku aja na kesi. **Kisw/Sanifu:** *Mshenga* wako kila siku anakuja na kesi.
6.	Mwana-mwali	40	45%	Mwari	49	55%	Mwari	**Zamani:** Mwanawe Asha ni *mwanamwali* nzima sasa. **Mabadiliko:** Mwanawe Asha ni *mwari* nzima sasa. **Kisw/Sanifu:** Mwanawe Asha ni *mwari* mzima kwa sasa.
7.	Pata-makamo	34	38%	Pataukubwa/ kuamwari/ kukua	55	62%	Kukua mwari	**Zamani:** Mwanangu *epatamakamo* tangu mwaka. **Mabadiliko:** Mwanangu ekuwa *mwari/epataukubwa* tangu mwaka jana. **Kisw/Sanifu:** Mwanangu amekuwa *mwari/amekuwa* tangu mwaka jana.

Matokeo ya utafiti katika jedwali 4.1 yanaonesha kuwa msamiati unatumika kabla ya harusi upo katika nyanja mbili. Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia ndogo umebadilika lakini kwa asilimia kubwa bado watu wanautumia kama ulivyo. Jumla ya msamiati 3 kati ya 7 sawa na 42.86% imeonekana kubadilika kwa asilimia ndogo. Msamiati huo ni "*chunguuwa*" (kutafuta siri ama kupeleleza au kutafuta ukweli wa mambo katika mbinu zako zote), bado unaumika kwa 60% na asilimia 40% wanasema "*chunguuza"*. Pia msamiati *"Dunga"* (kupitisha kitu kama vile uzi kwenye tundu ya kitu mfano; shanga, samaki na mauwa) nao unatumika kwa 54% na wahojiwa 46% wanasema *"tunga*". Imegundulika kuwa msamiati "dunga" ni miongoni mwa msamiati wa Kipemba uliyobadilika kiisimu/kilughawia, kwenye baadhi ya msamiati ya zamani yenye herufi "**d"** sasa wanaweka "**t"**. Mfano ***d****unga* - **t**unga, ***d****utu* - **t**utu, ***d****imka* - **t**imka, ***d****udumka* - **t**utumka, ***d****umbwikia* - **t**umbwikia na msamiati *"kukata mahari*" bado unatumika kwa 53% na 47% wanasema *"kudai mahari"* (kitendo cha kukasimu kiasi cha kiwango cha mahari).

Pia nyanja ya pili ni msamiati ambao umebadilika kwa kiasi kikubwa miongoni mwa Wapemba wenyewe na asilimia ndogo ya Wapemba bado wanautumia kama ulivyokuwa zamani, msamiati huu ulikuwa 4 kati ya 7 sawa na 57.14%. Msamiati wenyewe ni *"kifungua nlyango*" kwa sasa umekuwa *"kifungua mlango"* (sehemu ya mahari, mposaji anayotoa ili mwanamke atakaemuoa asipokelewe mahari kutoka kwa mume mwingine) kwa sasa zaidi ya Wapemba 64% wanautumia hivyo. Utamkaji wa kiisimu wa silabi "**la**" hapo asili wakitamka "**lya**" mfano *ku****lya*** baada ya ku**la**, ***lyaly****a* baada ya **lala** na mingineo. Pia msamiati *"mposi"* (mjumbe anaepeleka posa), hutumika kwa zaidi ya 54% badala ya maana ya zamani ya

“mposhi”. Pia *“Mwanamwali”* (ni msichana aliyekwisha baleghe lakini bado hajaolewa) kwa sasa *“mwari”* kwa 55% na, *“pata makamo”* (ni kitendo cha kubaleghe kwa msichana) umebadilika na kuwa *“kukuwa mwari”* au “*pata ukubwa*” kwa asilimia 62%.

Hivyo msamiati wote ulioainishwa ambao unatumika kabla ya harusi ulikuwa 7. Kati ya 7 ni msamiati 6 imebadilika na kuwa sawa na Kiswahili sanifu sawa na 85.71% ambayo ni *chunguuwa* - chunguuza, *dunga* - tunga, *kifunguanlyango* - kifunguamlango, *kukatamahari* - kudai mahari, *mwanamwali* - mwari na *patamakamo* - pataukubwa ama kuwamwari. Na msamiati 1 tu umebadilika katika hali tofauti, m*poshi* - mpos*i* - sawa na asilimia 14.29%.

4.2.1.2 Msamiati Unaotumika Wakati wa Harusi

Msamiati huu hutumika pale harusi inapofanyika ambapo mkusanyiko wa watu tayari umekusanyika kufanikisha harusi ile. Data hizi zilipatikana kwa njia ya usaili, hojaji na maelezo kupitia kwa watafitiwa wa kundi la vijana na wazee.

Jedwali Na. 4.2: Msamiati Unaotumika Wakati wa Harusi

Na		Msamiati						Mfano wa sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asili mia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asili mia**	**Kisw/Sanifu**	
1.	Changi	66	74%	Nchango/ mchango	23	26%	Mchango	**Zamani:** Mie sina bahati ya kupewa *changi ni ntu.* **Mabadiliko:** Mie sina bahati ya kupewa *nchango/mchango na ntu.* **Kisw/Sanifu:** Mie sina bahati ya kupewa *mchango na mtu.*
2.	Danda	46	52%	Ngaa/ngara	43	48%	Ngara	**Zamani:** Uharusi un'kupenda kwani twakuona **Mabadiliko:** Uharusi u'nkupenda kwani twakuona *wangaa/wangara*. **Kisw/Sanifu:** Uharusi umekupenda kwani unaonekana *unangara*.
3.	Kama/ utunda	19	21%	Ushanga	70	79%	Shanga	**Zamani:** Somoye harusi, *kama/utunda* za bi harusi zi wa? **Mabadiliko:** Someye harusi, *shanga* za bi harusi zi wa? **Kisw/Sanifu:** Somo yake bi harusi, *shanga* za bi harusi ziko wapi?
4.	Kiruruto	38	43%	Kigeregere	51	57%	Kigelegele	**Zamani:** Harusi ya leo inchanganka kwa *viruruto* **Mabadiliko:** Harusi ya leo inchanganka kwa *vigeregere*. **Kisw/Sanifu:** Harusi ya leo imechangamka kwa *vigelegele*
5.	Kyuo	39	44%	Chuo	50	56%	Chuo	**Zamani:** Nnapata *kyuo* kimoja tu hadi nnakonga. **Mabadiliko:** Nnapata *chuo*kimoja tu hadi nnakonga. **Kisw/Sanifu:** Nimepata *chuo* kimoja tu hadi nimezeeka
6.	Mbanjo	51	57%	Sanduku	38	43%	Sanduku/ begi	**Zamani:** *Mbanjoze pya zinaibwa.* **Mabadiliko:** Sandukule pya linaibwa. **Kisw/Sanifu:** Sanduku/begi lake lote limeibiwa.
7.	Ntoto	37	42%	Mwari	52	58	Bikira	**Zamani:** Nke wangu wa kwanza nnankuta ntoto **Mabadiliko:** Nke wangu wa mwanzo nnankuta mwari. **Kisw/Sanifu:** Mke wangu wa mwanzo nimemkuta bikira**.**

Matokeo katika jedwali 4.2 yanaonesha kuwa msamiati unatumika wakati wa harusi upo katika nyanja mbili vilevile kimabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia ndogo umebadilika lakini kwa asilimia kubwa bado unatumika kama ulivyo. Msamiati 3 kati ya 7 sawa na 42.86% iligundulika katika hali hiyo. Msamiati huo ni *"changi"* bado unatajwa kwa asilimia 69% ukilinganisha na "*nchango/mchango"* (mchango unaotolewa kwa ajili ya harusi inaweza kuwa pesa, nguo, kanga, vyakula na vyinginevyo,) hutumika kwa asilimia 31%. Pia msamiati *"danda"* (ni kitendo cha mtu kunawiri na kupendeza) ambapo hutumika 52% kuliko *"ngara"*. Vilevile *"mbanjo"* (ni zawadi ya nguo na vitu mbalimbali anavyopewa biharusi kutoka upande wa mume wake) unatumika zaidi *"mbajo"* kwa asilimia 57% badala ya *"sanduku"* ama *"begi".*

Pia Nyanja ya pili ni msamiati ambao umebadilika kwa kiasi kikubwa miongoni mwa Wapemba wenyewe na asilimia ndogo ya Wapemba bado wanautumia kama ulivyokuwa zamani. Hii uligundulika msamiati 4 kati ya 7 sawa na 57.14%. Msamiati huo ni *"kigeregere"* (sauti ya furaha inayotolewa na wanawake agh. harusini), hutumika zaidi kwa asilimia 57% badala ya *"kiruruto*", "chuo" (ni idadi ya mara alizoolewa mtu), unatumika kwa 56% badala ya *"kyuo"*. Pia msamiati huu umebadilika kiisimu, zamani herufi *"**ch**"* ilikuwa si aghlabu kutumika na badala yake hutumika *"**ky**"* mfano **ky**ura badala ya **ch**ura, **ky**a badala ya **ch**a, **ky**ungu badala ya **ch**ungu, **ky**angu badala ya **ch**angu na mingineyo. Pia *"mwari/bikira"* (bi harusi ambaye ni bikira yaani na hajawahi kufanya tendo la ndoa) unatumika zaidi kwa 58% badala ya *"ntoto*". Msamiati *"shanga"* (ushanga

unaovaliwa na wanawake kiunoni kama pambo) unatumika kwa asilimia 79% badala ya *"kama/utunda"* ulivyokuwa ukizungumzwa zamani.

Hivyo msamiati wote ulioainishwa ambao unatumika wakati wa harusi, imegundulika kuwa msamiati wote unabadilika kuelekea Kiswahili sanifu kwa asilimia 100%. Tukiangalia maneno hayo ni *changa* - mchango, *danda* - ngara, *kama/utunda* - ushanga, *kiruruto* - kigeregere, *kyuo* - chuo, *mbanjo* - sanduku/begi na *ntoto* - bikira.

4.2.1.3 Msamiati Unaotumika Baada ya Harusi

Huu ni msamiati ambao mara nyingi hutumika wakati harusi imekwishafanyika. Inawezekana ikawa muda mfupi au muda mrefu tangu wawili wale waoane. Data hizi zilipatikana kutokana kwa watoa taarifa wakiwemo wazee na vijana kupitia hojaji, usaili na maelezo, kama inavyooneshwa kwenye jedwali 4.3 hapo chini.

Jedwali Na. 4.3: Msamiati Unaotumika Baada ya Harusi

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Kisw/Sanifu**	
1.	Bankwe	46	52%	Nkwe/ Mkwe	43	48%	Baba mkwe	**Zamani:** *Bankwe* wangu leo aumwa mperesha. **Mabadiliko:** *Nkwe/mkwe* wanguaumwa mperesha. **Kisw/Sanifu:** *Mkwe* wangu anaumwa na presha.
2.	Mankwe	46	52%	Mama-mkwe/	43	48%	Mama mkwe	**Zamani:** *Mankwe* wangu leo asafiri. **Mabadiliko:** *Nkwe* wangu leo asafiri. **Kisw/Sanifu**: Leo *Mama mkwe* wangu anasafiri.
3.	Nkazahau	14	16%	Mkwe/ nkwe	75	84%	Mkwe	**Zamani:** Yule ni *nkazahau* wangu. **Mabadiliko:** Yule *mkwe* wangu. **Kisw/Sanifu:** Yule ni mkwe wangu.
4.	Utuume	45	51%	Ujana-dume	44	49%	Uwanaume	**Zamani:** Apenda oa wala hana *utu uume*. **Mabadiliko:** Apenda oa wala hana *ujana dume.* **Kisw/Sanifu:** Anapenda kuoa wala hana *uwanaume*.
5.	Uili	41	46%	Uwili/	48	54%	Wake wawili	**Zamani:** Babaye ana *uili*. **Mabadiliko:** Babaye ana *uwili.* **Kisw/Sanifu**: Baba yake ana *wake wawili.*

Matokeo katika jedwali 4.3 yanaonesha kuwa msamiati unatumika baada ya harusi upo katika nyanja mbili vilevile katika mabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia ndogo umebadilika lakini kwa asilimia kubwa bado unatumika kama ulivyo. Msamiati 3 kati ya 5 sawa na 60% iligundulika katika hali hiyo. Msamiati huo ni *"bamkwe"* (baba wa mke au mume wa mtu) pia *"mankwe*" (mzazi wa mke wako ama mzazi wa mume wako), msamiati huu unatumika kwa asilimia 52%. Pia *"utuume"* (uwezo wa mwanamme kutunza mke) hutumika kwa asilimia 51% na 49% hutumia katika mabadiliko *"ujanadume"*

Pia Nyanja ya pili ni msamiati ambao umebadilika kwa kiasi kikubwa na asilimia ndogo ya Wapemba bado wanautumia kama ulivyokuwa zamani. Hii uligundulika msamiati 2 kati ya 5 sawa na 40%. Mfano wa msamiati huo ni *"uwili"* (ndoa ambayo mume ana wake wawili) hutumika kwa asilimia 54% badala ya *"uili"* vilevile msamiati *"nkazahau*" (mke wa mjomba) umebadilika kwa asilimia nyingi sawa na 84% na kuwa *"mkwe/nkwe".*

4.2.2 Msamiati wa Msibani

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) na TUKI (2004) wameeleza kuwa msiba ni tukio la maafa linalomfanya mtu kuwa na hudhuni. Ni tukio kama vile kufiwa, kupotelewa na mali au hata tukio la maafa makubwa linalomfanya mtu ahudhunike sana. Hivyo mtafiti ameukusanya msamiati wa msibani tu. Kifo ni tukio la mtu au kiumbe chochote chenye uhai kuaga dunia (kufariki). Mara nyingi watu wanaoathirika sana na msiba huu ni watu wa karibu na marehemu mfano; baba, mama, mtoto na hata

marafiki na wingineo. Msamiati wa msibani umegawika katika mikabala mitatu kimatumizi yaani kabla, wakati na baada ya msiba kama ifuatavyo:

4.2.2.1 Msamiati Unaotumika Kabla ya Msiba

Msamiati huu hutumika pale panapokuwa pana mgonjwa taabani wa kukatiwa tamaa au njozinjozi za kutaka kupita kwa tukio la msiba huo. Data hizi zilikusanywa katika vyanzo tofauti vikiwemo hojaji, usaili na maelezo kutoka kwa watafitiwa wenyewe ambao ni wazee na vijana. Tafsiri zilizotolewa kwenye uchambuzi zimepatikana kutoka katika kamusi ya Bakhressa (1992), BAKIZA (2014) na TUKI (1984) kama ilivyochambuliwa hapo chini.

Jedwali Na. 4.4: Msamiati Unaotumika Kabla ya Msiba

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asili mia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Adi	11	12%	Ndwele	78	88%	Ugonjwa /maradhi	**Zamani:** Eshikwa ni *adi /ndwele* hadi umautiwe. **Mabadiliko:** Eshikwa ni *ndwele* hadi umautiwe. **Kisw/Sanifu:** Ameshikwa na *maradhi/ugonjwa* hadi umauti wake.
2.	Agadunia	40	45%	Kufa/ Kufariki	49	55%	Kufa/ Kufariki	**Zamani:** N'gonjwa wao *kanaaga dunia* jana usiku. **Mabadiliko:** N'gonjwa wao *kankufa/kanfariki* jana usiku. **Kisw/Sanifu:** Mgonjwa wao *kafa/kafariki* jana usiku.
3.	Powa	42	47%	Kantuto ka/katut oka	47	53%	Katutoka	**Zamani:** Yule n'gonjwa wetu *kampowa*. **Mabadiliko**: Yule mgonjwa wetu *kantutoka/katutoka.* **Kisw/Sanifu:** Yule mgonjwa wetu *keshafariki/keshakufa.*
4.	Uchimvi	58	65%	Uchuro	31	35%	Uchuro	**Zamani:** Jana watoto wamfanya *uchimvi* ta, leo tun'filiwa. **Mabadiliko:** Jana watoto wamfanya *uchuro* ta, leo tun'filiwa **Kisw/Sanifu:** Jana watoto wamefanya *uchuro* hata, leo tumefiliwa

Matokeo katika Jedwali 4.4 yanaonesha kuwa msamiati unatumika kabla ya msiba upo katika nyanja mbili vilevile kimabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia kubwa umebadilika na kuwa na maana mpya, lakini kwa asilimia ndogo bado unatumika kama ulivyo. Msamiati 3 kati ya 4 sawa na 75% iligundulika katika hali hiyo. Msamiati huo ni *"adi"* (kitendo cha maradhi makubwa ambayo husababisha mtu kufa), huu umebadilika kwa asilimia 88% na kuwa *"ndwele"*, msamiati *"aga dunia"* (kitendo cha kuondoka duniani/kutokwa na roho) kwa sasa zaidi unatumika *"kufa ama kufariki"* kwa asilimia 55% na *"powa"* (neno linalotumika kumpa mtu habari ama taarifa ya kifo) limebadilika kwa asilimia kwa 53% na kuwa *"katutoka"*

Pia Nyanja ya pili ni msamiati ambao umebadilika kwa kiasi kidogo miongoni mwa Wapemba wenyewe na asilimia kubwa ya Wapemba bado wanautumia kama ulivyokuwa zamani. Hii uligundulika msamiati 1 kati ya 4 sawa 25% ambao ni *"uchuro"* (jambo ambalo kutokea kwake huwa ni ishara ya janga) bado watu wingi wanalitumia neno "*uchimvi"* kwa asilimia 58%.

4.2.2.2 Msamiati Unaotumika Wakati wa Maziko

Msamiati huu hutumika pale watu wanapokuwa katika harakati za mazishi. Kuanzia kumshughulikia maiti mpaka kumtia kaburini kwake. Msamiati huu umeweza kukusanywa kwa kutumia hojaji, usaili pamoja na maelezo kupitia makundi yote yaliyolengwa ambayo ni vijana na wazee. Uainishaji wake umeoneshwa na jedwali 4.5 hapa chini.

Jedwali Na. 4.5: Msamiati Unaotumika Wakati wa Maziko

Na	Msamiati							Mfano wa sentensi
	Msamiati wa Awali	**Kiw Cha Mat**	**Asili mia**	**Msamiati Mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Kiunza	23	26%	Ubao	66	73%	Ubao	**Zamani:** *Kiunza* tunkisahau nyumbani. **Mabadiliko:** *Ubao* tushausahau nyumbani **Kisw/Sanifu:** *Ubao* tumeusahau nyumbani
2.	kupamba	43	48%	Kafini	46	52%	Kuvisha sanda	**Zamani:** Wakati wendavye njooni *tumpambe* maiti tukanzike. **Mabadiliko:** Wakati wendavye njooni *tunkafini* maiti tukanzike. **K/Sanifu:** Wakati unakwenda zake njoonit u*mvishe sanda* maiti tukamzike.
3.	Mava	55	62%	Makaburini	34	38%	Makaburini	**Zamani:** *Mava yetu i* Kinondoni. **Mabadiliko:** *Makaburi* yetu ya Kinondoni. **Kisw/Sanifu**: *Makaburi* yetu yapo Kinondoni.
4.	Tusi	32	36%	Jeneza	57	64%	Jeneza	**Zamani:** Maiti intiwa *tusini* mapema. **Mabadiliko:** Maiti intiwa *jenezani* mapema. **Kisw/Sanifu:** Maiti imetiwa kwenye *jeneza* mapema.
5.	Vifiwa	44	49%	Vizikwa	45	51%	Mchango	**Zamani:** Kuntoa *vifiwa*? **Mabadiliko:** Kuntoa *vizikwa*? **Kisw/Sanifu:** Kushatoa *mchango wa msiba*?

Matokeo katika Jedwali 4.5 yanaonesha kuwa msamiati unatumika wakati wa maziko upo katika nyanja mbili vilevile kimabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia kubwa umebadilika miongoni mwa watumizi wake. Msamiati 4 kati ya 5 sawa na 80% iligundulika katika hali hiyo. Msamiati huo ni *"ubao"* hutumika kwa asilimia 73% badala ya *"kiunza"* (ubao unaofunikiwa maiti kwenye mwanandani kaburini). Pia msamiati *"tusi"* umepungua nguvu kutajwa na sasa wingi wanasema *"jeneza"* (kitanda au kilili maalumu cha kuchukulia maiti kumpeleka kaburini) kwa asilimia 64%, pia *"vizikwa"* (pesa anazopewa mfiwa kumfariji) unatumika kwa asilimia 51% ukilinganisha na wazamani *"vifiwa"* pamoja na msamiati *"kupamba"* (kuvisha sanda maiti) kwa sasa watu wingi wanautaja *"kafini"* kwa asilimia 52%.

Umegundulika msamiati mmoja (1) tu ambao umebadilika kwa kiasi kidogo miongoni mwa Wapemba wenyewe na asilimia kubwa ya Wapemba bado wanautumia kama ulivyokuwa zamani sawa na asilimia 20%, msamiati wenyewe ni *"mava"* (pahali maalumu wanapozikwa watu), bado kwa asilimia 62% unatumika hivyo na asilimia 38 % wanasema *"makaburini*".

4.2.2.3 Msamiati Unaotumika Baada ya Msiba

Huu ni msamiati unaotumika baada ya maiti kwenda kuzikwa na kadiri ya wakati unavyoendelea baada ya kifo chake**.** Utafiti uligundua yafuatayo kama jedwali 4.6 linavyodhihirisha.

Jedwali Na. 4.6: Msamiati Unaotumika Baada ya Msiba

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Hayati	31	35%	Marehemu	58	65%	Marehemu	**Kipemba:** *Hayati* Karume kanauliwa m'magaidi. **Mabadiliko:** *Marehemu* Karume kanauliwa m'magaidi. **Kisw/Sanifu:** *Marehemu* Karume ameuliwa na magaidi.
2.	Mwana -mkiwa	09	10%	Yatima	80	90%	Yatima	**Zamani:** Uyo *mwanankiwa* yu wa? **Mabadiliko:** Uyo *yatima* yu wa? **Kisw/Sanifu:** Huyo *yatima* yuko wapi?
3.	Kuinua-tanga	35	39%	Kutawa-nyika	54	61%	Kutawa-nyika	**Zamani**: *Twainua tanga* Ijumaa. **Mabadiliko:** *Twatawanyika* siku ya Ijumaa. **Kisw/Sanifu:** *Tunatawanyika* siku ya Ijumaa.

Matokeo katika jedwali 4.6 yanaonesha kuwa msamiati unatumika baada ya msiba umebadilika kimatumizi na kuwa sawa na Kiswahili sanifu kwa asilimia 100%. Msamiati hiyo ni *"hayati"* umekuwa *"marehemu"* (neno linalotumika kumtaja mtu aliefariki) kwa 65%. Pia *"mwanamkiwa"* umekuwa *"yatima"* (mtoto aliyefiwa na baba yake) kwa 90% na neno *"kuinua tanga"* limekuwa *"kutawanyika"* (ni kitendo cha wahusika au wafiwa kuondoka sehemu ya msibani baada ya siku tatu ama zaidi kufika tangu msiba utokee) nao umebadilika kwa asilimia 61%.

4.2.3 Msamiati wa Uvuvini

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), uvuvi ni kazi ya kwenda kutafuta samaki kama vile baharini, mtoni au ziwani. TUKI (2004) nalo imeeleza kuwa uvuvi ni kazi ya kuvua samaki. Hivyo neno uvuvini ni sehemu inayofanyika kazi ya uvuvi. Mtafiti ameugawa msamiati wa uvuvini katika makundi matatu kimatumizi yaani majina ya samaki, majina ya vitu vya uvuvini na vitendo vya uvuvini kama ifuatavyo;

4.2.3.1 Msamiati wa Majina ya Samaki

Msamiati wa majina ya samaki ni majina yanayotambulisha jinsi ya uitwaji wa samaki. BAKIZA (2012) imefasili majina ya aina za samaki kama inavyoonesha hapo chini. Data hizi pia zilikusanywa kutoka kwa wazee na vijana kupitia zana zao za maswali yaliyoandaliwa na mtafiti.

Jedwali Na. 4.7: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Samaki

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**		**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**		**K/Sanifu**	
1.	Fufu	46	52%	Ng'ombe-bahari	43	48%	Kigombe gombe	**Zamani:** Samaki nimpendae *nfufu.* **Mabadiliko:** Samaki nimpendae *n'ng'ombe bahari.* **Kisw/Sanifu:** Samaki nnaempenda ni *ng'ombe bahari*.
2.	Fujwe/nyimbi	41	46%	Perege	48	54%	perege	**Zamani**: Samaki wa *funjwe* ladhaye si watamu. **Mabadiliko:** Samaki wa *perege* ladhaye si tamu. **Kisw/Sanifu:** Samaki wa *funjwe* ladha yake si tamu.
3.	Gongea	45	51%	Mkizi	44	49%	Mkizi	**Zamani:** Ugali kwa *gongeoni* ni ntamu. **Mabadiliko:** Ugali kwa *gongeo* ni ntamu. **Kisw/Sanifu:** Ugali kwa *mkizi* ni mtamu
4.	Kyambuzi	39	44%	Kiambuzi	50	56%	Dokozi	**Zamani:** Usiwe n'janja kama *kyambuzi*. **Mabadiliko:** Usiwe n'janja kama *kiambuzi*. **Kisw/Sanifu:** Usiwe mjanja kama *dokozi*.
5.	Shaza	30	34%	Chaza	59	66%	Chaza	**Zamani:** *Shaza* ni nzuri kwa kuunga nchuzi. **Mabadiliko:** *Chaza* ni wazuri kwa kupikamchuzi. **Kisw/Sanifu:** *Chaza* ni wazuri kwa kupika mchuzi.

Matokeo katika Jedwali 4.7 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika majina ya samaki upo katika nyanja mbili vilevile kimabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia ndogo umebadilika na asilimia kubwa ya watumiaji wake bado wanautumia kama zamani. Kati ya msamiati 5 iliyokusanywa, msamiati 2 iligundulika kuwa hivyo sawa na 40%. Msamiati wenyewe ni samaki aina ya *"fufu"* unatumika kwa asilimia 52% licha ya msamiati *"ng'ombe bahari"* (samaki wa wastani mwenye umbo la kisanduku na mdomo mdogo wa duara) unaotumika kwa asilimia 48% na *"gongea"* unatumika kwa 51% ukilinganisha na *"mkizi"* (samaki wa kiasi, mweupe mwenye magamba).

Msamiati ambao kwa asilimia kubwa ya watumizi wake umebadilika ilikuwa 3 sawa na 60%. Msamiati huo ni *"kyambuzi"* (Samaki mdogo anaekula chambo bila ya kunasa) umekuwa *"kiambuzi"* kwa asilimia 56%, *"chaza"* (kiumbe cha pwani jamii ya panga, chenye umbo bapa) unatumika kwa asilimia 66% badala ya *"shaza" na perege* (Samaki wa wastani wa maji baridi, anaefanana na gongeo, mwenye magamba yanayong'ara) hutumika kwa asilimia 54% badala ya *"funjwe/nyimbi"*

4.2.3.2 Msamiati wa Majina ya Vitu vya Uvuvini

Majina ya uvuvini ni majina yanayotaja na yanayojuulisha vitu vitumikavyo katika harakati za uvuvi. Vinaweza vikawa zana za uvuvini, vyombo vya baharini na vitu vilivyozunguka. Data hizi pia zilipatikana kutoka katika makundi yote yaliyotafitiwa ambayo ni kundi la wazee na vijana. Katika ukusanyaji wa data hizi maswali ya hojaji, usaili pamoja na maelezo yalitumika kufanikisha kupata data hizi.

Jedwali Na. 4.8: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Vitu vya Uvuvini

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/sanifu**	
1	Chaawe	38	43%	Matumbawe	51	57%	Matumbawe	**Kipemba:** Nyavu zetu zinkwama kwenye *chaawe*. **Mabadiliko:** Nyavu zetu zinkwama kwenye *matumbawe.* **Kisw/Sanifu**: Nyavu zetu zimekwama kwenye *matumbawe.*
2	Kichapwa	47	53%	Gwandi	42	47%	Uzio	**Zamani:** *Kichapwa* changu kintoboka. **Mabadiliko:** *Kichapwa* changu kintoboka. **Kisw/Sanifu:** *Uzio* wangu umetoboka.
3	Forozani/gatini	31	35%	Bandarini	58	65%	Gatini/bandarini	**Kipemba:** N'nda *forozani* kuchukua nzigo wangu. **Mabadiliko:** Nnda *gatini/bandarini* kuchukua nzigo wangu. **Kisw/Sanifu:** Nnakwenda *forozani* kuchukua nzigo wangu.
4	Lema	19	21%	Dema	70	79%	Dema	**Kipemba:** Kitatange kin'ngia *lemani* **Mabadiliko:** Kitatange kin'ngia *demani.* **Kisw/Sanifu:** Kitatange kimeingia kwenye *dema.*
5	Shumbwi	28	32%	Chubwi	61	68%	Chubwi	**Kipemba:** *Shubwi* zetu zote za kuvuliazim'maliza. **Mabadiliko:** *Chubwi* zetu zote za kuvulia zim'maliza. **Kisw/Sanifu:** *Chubwi* zetu zote za kuvulia zimemaliza.

Matokeo katika Jedwali 4.8 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika majina ya vitu vya uvuvini upo katika nyanja mbili vilevile kimabadiliko ya kimatumizi.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao kwa asilimia kubwa umebadilika na kuwa na matumizi sawa na Kiswahili sanifu, msamiati 4 kati ya 5 sawa na 80% iligundulika katika hali hiyo. Msamiati hio ni *"chaawe"* (jiwe laini la mwamba wa baharini lakini kubwa sana) umebadilika na kuwa *"matumbawe"* kwa asilimia 57%, pia *"gatini/forozani*" (mahali maalumu karibu na eneo la bahari ambapo bidhaa zinaingia na kutoka na vyombo vya usafiri vinapatikana) umebadilika kwa asilimia 65% na kuwa *"bandarini"* na msamiati *"lema"* (mtego wa samaki unaofumwa kwa matete au vijiti) umebadilika na kuwa *"dema"* kwa asilimia 79% na neno *"shumbwi"* (kitu kizito kinachofungwa kwenye mshipi wa kuvulia samaki) umebadilika na kuwa *"chubwi"* kwa 68%.

Pia Nyanja ya pili ni msamiati ambao umebadilika lakini bado Wapemba wingi wanautumia kama zamani. Hii uligundulika msamiati mmoja (1) kati ya 5 sawa na 20%. Msamiati huo ni *"kichapwa"* badala ya *"uzio"* (namna ya boma la miti la kuzuia samaki wakamatwe wakati wa maji yanapotoka/yanapokupwa baharini), msamiati huo kwa 53% bado unatumika *"kichapwa"*

4.2.3.3 Msamiati Unaoonesha Vitendo vya Uvuvini

Ni msamiati unaoonesha ufanyikaji wa mambo yote ya vitendo katika kufanikisha tendo zima la harakati za kiuvuvi au mambo ya usafiri kupitia baharini**.** Msamiati huu ulipatikana kwa kutumia zana za hojaji, usaili na maelezo, kwa kundi la wazee na vijana. Maana zote hizo zimepatikana kutoka BAKIZA (2012)**.**

Jedwali Na. 4.9: Msamiati Unaotumika Kuonesha Vitendo vya Uvuvini

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha**	**Asili mia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Chasha	32	36%	Vuusha	57	64%	Vusha	**Zamani:** Babu Hamadi *tushachishe* watuchelewa. **Mabadiliko:** Babu Hamadi *tuvuushe* watuchelewesha. **Kisw/Sanifu:** Babu Hamadi *tuvuushe* unatuchelewesha.
2.	Dota	42	47%	Dona	47	53%	Donoa	**Zamani:** Leo samaki *hewedota* kwenye nshipi wangu. **Mabadiliko:** Leo samaki *hewedona* nshipi wangu. **Kisw/Sanifu**: Leo samaki *hawakudonoa* kwenye mshipi wangu.
3.	Limbua	47	53%	Zongomoa	42	47%	Zongoa/ gandua	**Zamani:** N'nda limbua nyavu yangu. **Mabadiliko:** N'nda zongoa nyavu yangu. **Kisw/Sanifu:** Ninakwenda *kuzongo/kugandua* nyavu yangu.

Matokeo katika Jedwali 4.9 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika majina ya vitendo vya uvuvini upo katika nyanja mbili.

Nyanja ya kwanza ni msamiati ambao umebadilika kwa kiwango kikubwa miongoni mwa watumiaji wake. Msamiati 2 kati ya 3 sawa na 66.67% iligundulika katika hali hiyo, nao ni *"chasa"* kwa sasa watumiaji wingi wastani wa 64% wanautumia kama *"vusha"* (kitendo cha kupitisha kitu au mtu kutoka ng'ambo moja hadi nyingine kwa kutumia vyombo vidogovidogo vya baharini). Vilevile msamiati *"dota"* (kitendo cha samaki kudonoa chambo kilichomo kwenye ndoana iliyopo ncha ya mshipi) kwa sasa unatumika *"dona/donoa"* kwa asilimia 53%.

Nyanja ya pili ni msamiati ambao Wapemba wingi wanautumia katika matumizi ya zamani. Msamiati mmoja (1) kati ya 3 umeonekana kuwa hivyo sawa na asilimia 33.33%. Msamiati wenyewe ni *"limbua"* (ni kitendo cha mtu kugandua nyavu iliyokwama chini baharini) badala ya *"zongomoa/gandua"* msamiati mpya.

4.2.4 Msamiati wa Kilimoni

Kwa mujibu wa TUKI (1981), kilimo ni shughuli za kulima kwa utaratibu wa kutumia zana za kulimia, kama jembe la mkono au pilau na Bakhressa (1992) amesema kilimo ni kazi ya kulima. Kwa hivyo kilimo ni kitendo cha kazi yakupanda, kuimarisha au kustawisha mimea kwenye ardhi. Mtafiti ameugawa msamiati wa kilimo katika matumizi matatu kama ifuatavyo; Msamiati wa majina ya mimea, vifaa vya kilimo na vitendo katika kilimo.

4.2.4.1 Msamiati wa Majina ya Mimea

Msamiati huu unaonesha mtajo wa mimea tu inayopatikana kisiwani Pemba. Msamiati huo umepatikana kutoka kwa watafitiwa wenyewe na maana zote hizo hapo chini zimetoka katika kamusi la lahaja ya Kipemba, BAKIZA (2012).

Jedwali Na. 4.10: Msamiati Unaotumika katika Majina ya Mimea

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Mbono	62	70%	Mbarika	27	30%	Mbarika	**Zamani:** *Mbono* ni nzuri kwa kukandiya. **Mabadiliko:** *Mbarika* ni nzuri kwa kukandiya. **Kisw/Sanifu:** *Mbarika* ni mzuri kwa kukandiya.
2.	Nriba	58	65%	Ntoriro	31	35%	Mtoriro /Matembere	**Zamani**: Leo napika *nriba* na masheli. **Mabadiliko:** Leo napika *ntoriro* na masheli. **Kisw/Sanifu:** Leo napika *mtoriro/matembele* na mashelisheli.
3.	Ntunda	45	51%	Mwarubaini	44	49%	Mwarubaini	**Zamani:** Nchumie *ntunda* tumbo laniuma. **Mabadiliko:** Nchumie *mwarubaini* tumbo laniuma. **Kisw/Sanifu:** Nichumie *mwarubaini* tumbo linaniuma.
4.	Nzumari	49	55%	Nchainchai/mchaichai	40	45%	Mchaichai	**Kipemba:** Chai ya *nzumari* yanukia vizuri. **Mabadiliko**: Chai ya *nchaichai* yanukia vizuri. **Kisw/Sanifu:** Chai ya *mchaichai* inanukia vizuri.

Matokeo katika Jedwali 4.10 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika majina ya mimea upo katika katika nyanja moja tu. Nyanja ambayo msamiati wake kwa asilimia ndogo umebadilika lakini kwa asilimia kubwa kwa Wapemba wanautumia kama zamani. Msamiati huo ni *"mzumari"* unatumika kwa asilimia 55% ingawa asilimia 45 wanautumia kwa jina la *"mchaichai"* (mmea mfupi wenye majani membamba marefu yenye harufu nzuri, yanayotumika kama kiungo agh. kwenye chai). *"Mbono"* (mmea wa wastani wenye majani mapana na tunda zinazolevya, za kijani zenye mbegu zilizofanana na kunde) pia hutumika kwa asilimia 70% dhidi ya msamiati *"mbarika", "mriba/nriba"* (mmea unaotambaa, wenye majani jamii ya viazi, yaliyogawika katika pandapanda na hutumika kama mboga) neno *"mriba"* linatumika zaidi ukilinganisha na neno *"mtoriro/mriba"* kwa asilimia 65% na msamiati *"mtunda/ntunda"* (mti mkubwa wenye matawi mingi, majani madogo yenye kingo za msumeno na tunda za manjano unaotumika kuwa ni dawa ya maradhi mbalimbali) badala ya *"mwarubaini"* kwa asilimia 51%.

4.2.4.2 Msamiati wa Vifaaa Vinavyotumika Kilimoni

Msamiati huu huonesha tamko la vifaa vya kilimoni, aidha ni zana, aina za mazao na matunda na vitu vilivyozunguka mazingira hayo. Msamiati huu ulipatikana kwa kutumia zana ya hojaji, usaili na maelezo katika makundi yote yaliyotafitiwa.

Jedwali Na. 4.11: Msamiati Unaotumika katika Majina yaVitu vya Kilimoni

Na	Msamiati							Mfano wa Sentensi
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha**	**Asilimia**	**K/Sanifu**	
1.	Kandoro	08	09%	Viazi vitamu	81	91%	Viazi vitamu	**Zamani**: Nsimu huu *kandoro* vina mafunza. **Mabadiliko:** Nsimu huu *viazi vitamu* vina mafunza. **Kisw/Sanifu:** Msimu huu *viazi vitamu* vina mafunza.
2.	Kitango - pepeta	12	13%	Kitango	77	87%	Kitango	**Kipemba**: Neumwa n'gesi, nkila *kitangopepeta* hapohapo hibesa. **Mabadiliko:** Neumwa n'gesi, nkila *kitango* hapohapo hibesa. **Kisw/Sanifu**: Niliumwa na gesi, nikala *kitango* hapoapo nilipona.
3.	Kyovyo	42	47%	Chovo	47	53%	Kingoe	**Zamani**: *Kyovo* changu munkiazima halafu hamwekirejesha tena. **Mabadiliko**: *Chovo* changu munkiazima halafu hamwekirejesha tena. **Kisw/Sanifu**: *Kingowe* changu mumekiazima halafu hamujakirejesha tena.
4.	Shoroko	38	43%	Choroko/ chooko	51	57%	Chooko	**Zamani:** Mara hii *shooko* zimvyaa sana. **Mabadiliko**: Mara ii *choroko/chooko* zimvyaa sana. **Kisw/Sanifu:** Mara hii *chooko* zimezaa sana.
5.	Tango	48	53%	Boga	51	57%	Boga	**Zamani:** Futari ya leo *ntango* na tambi. **Mabadiliko:** Futari ya leo *m'boga* na tambi. **Kisw/Sanifu:** Futari ya leo ni *boga* na tambi.

Matokeo katika Jedwali 4.11 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika vifaa vya kilimoni, takribani wote umebadilika na kuwa na matumizi sawa na Kiswahili Sanifu. Msamiati yote 5 imegundulika hivyo sawa na 100% Msamiati huo ni "kandoro" (kiazi kidogo kitamu) umebadilika na kuwa *"viazi vitamu"* kwa asilimia 91%, *"kitango pepeta"* (tunda dogo refu, mviringo linaoliwa bichi, jamii ya tango) umebadilika na kuwa *"kitango"* kwa asilimia 87%. Halikadhalika msamiati *"Shoroko/choroko"* umebadilika na kuwa *"chooko"* (aina ya nafaka za rangi ya kijani ya jamii ya kunde lakini ndogo zaidi) hutumika kwa asilimia 57%, pia *"kyovyo/chovyo"* (fimbo iliyopindwa nchani inayotumiwa kuinamishia tawi la mti ili kuchuma matunda) kwa sasa unatumika *"kingoe"* kwa asilimia 53% na msamiati *"tango"* (tunda kubwa la mviringo linaloliwa baada ya kupikwa, lenye gamba gumu linaloteleza, nyama yake rangi ya manjano na lina kokwa nyingi) hutumika *boga"* kwa sasa kwa asilimia 57%.

4.2.4.3 Msamiati wa Vitendo vya Kilimoni

Msamiati wa vitendo vya kilimoni ni msamiati unaoonesha jinsi utendaji wa shughuli hizo. Msamiati huu ulipatika kutoka kwa watafitiwa vijana na wazee.

Jedwali Na. 4.12: Msamiati Unaotumika KuoneshaVitendo vya Kilimoni

Na	**Msamiati**							**Mfano wa Sentensi**
	Msamiati wa awali	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**Msamiati mpya**	**Kiw Cha Mat**	**Asilimia**	**K/sanifu**	
1.	Bopa	44	49%	Bofya/ dosa	55	51%	Bofya	**Zamani:** *Libope* ilo papai linawiva. **Mabadiliko:** *Libofye* ilo papai limewiva. **Kisw/Sanifu:** *Libope* ilo papai lishawiva?
2.	Bwaga	51	57%	Angua	37	43%	Angusha	**Zamani:** N'nda *bwaga* nazi. **Mabadiliko:** N'nda *angusha* nazi. **Kisw/Sanifu:** Nnakwenda *kuangusha* nazi.
3.	Funda	48	54%	Twanga	41	46%	Twanga	**Zamani:** *Kaufunde* huwo mpunga tupate kijio. **Mabadiliko:** *Kaufunde* huo mpunga tupate kijio. **Kisw/Sanifu:** *Kautwange* huwo mpunga tupate chakula cha mchana.
4.	Pepetesa	32	36%	Pepeta/peta	57	64%	Peta	**Kipemba:** *Pepetesa* uwo mpunga. **Mabadiliko:** *Peta* huo mpunga. **Kisw/Sanifu:** *Peta* huo mpunga.

Matokeo katika Jedwali 4.12 yanaonesha kuwa msamiati unatumika katika majina ya vitendo vya kilimoni upo katika nyanja mbili. Upo msamiati 2 ambao unaonekana kuwa sawasawa na matumizi ya Kiswahili sanifu kati ya 4 sawa na 50%. Ambao ni *"bopa"* (kitendo cha mtu kugongagonga tunda kwa kidole ili kuliangalia kama limeiva) kwa sasa asilimia 51% wanasema *"bofya"* na "*pepetesa"* (rusharusha nafaka katika kitunga au ungo ili kuondosha makapi na takataka) kwa asilimia 64% kwa sasa wanasema *"pepeta/peta".*

Pili ni msamiati ambao umebadilika lakini Wapemba wingi bado wanautumia kama ulivyokua zamani. Hii nayo ilikuwa 2 kati ya 4 sawa na 50%. Msamiati wenyewe ni "bwaga" (angusha matunda kwa nguvu kutoka juu ya mti) unatajika kwa asilimia 57 dhidi ya msamiati mpya *"angusha"* na pia msamiati "*funda"* (kulainisha kitu kikavu na kuwa unga hasa katika aina za nafaka mpaka kilainike), unatajwa kwa asilimia 54 dhidi ya *"twanga"* ambao unatumika kwa 46%.

4.3 Kutathmini Tofauti ya Kiasi cha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati Kiasilimia

Lengo mahsusi la pili la utafiti ni kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni. Malengo haya yaliongozwa na swali la pili lililokuwa likiuliza; Kuna tofauti gani ya mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba uliojitokeza kiasilimia kulinganana muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni? Maoni ya watafitiwa yalibainisha tofauti hizo katika miktadha husika ikiongozwa na nadharia ya ubadilikaji ya Darwin (1838) kama ilivyoelezewa kwa kina uk.10. Msamiati huo ulikusanywa na kuainishwa kama inavyoonesha hapo chini:



Kielelezo Na. 4.1: Tofauti ya Mabadiliko ya Msamiati

4.3.1 Uchambuzi

Kwa mujibu wa data zilizopo hapo juu, jumla ya msamiati 57 uliokusanywa katika miktadha yote. Kati ya hiyo msamiati 19 ya muktadha wa harusini umebadilika katika matumizi yake sawa na asilimia 33.33%. Msamiati 12 ulikuwa wa muktadha wa msibani sawa na 21.05%, msamiati wa uvuvini ilikuwa 13 sawa na 22.81% halikadhalika na msamiati wa kilimoni ulikuwa 13 sawa na asilimia 22.81.

Kutokana na ulinganishi wa msamiati katika muktadha yote minne iliyolinganishwa, data zimedhihirisha kuwa msamiati wa harusini umebadilika zaidi ukilinganisha na muktadha wa msibani, kilimoni na uvuvini kwa asilimia 33.33%. Kati ya watafitiwa 89, watafitiwa 71 wamesema kuwa msamiati wa harusini unapokea mabadiliko haraka ukilinganisha na miktadha mingine sawa na asilimia 79.77%. Walisema sababu za muktadha huo kupokea mabadiliko haraka ni:

(i) Mitindo ya harusi inabadilika kutokana na wakati pamoja na mabadiliko ya kidunia. Mambo mapya yanayopendezesha sherehe za harusi yanazuka kila

kukicha vikiwemo vipambo, mavazi, vyakula, ngoma na mingineo. Pia wakasema msamiati wa harusini unakusanya watu wenye utamaduni mchanganyiko wakati wa sherehe ile.

(ii) Pia wakaeleza kuwa Wapemba wanaoa na kuolewa na watu wenye utamaduni tofauti.

(iii) Vilevile kupitwa na wakati kwa mila za zamani na kulazimika kuiga tamaduni zinazokwenda na wakati.

Watafitiwa 81 kati ya 89 sawa na 91.01%, walitoa maoni yao na kusema kuwa msamiati wa msibani unabadilika kwa kiwango kidogo ukilinganisa na muktadha wa harusini, kilimoni, na uvuvini. Pia maoni ya watafitiwa yamekwenda sawa na data zilizoonesha kuwa msamiati wa msibani unabadilika kwa asilimia 21.05%. Watafitiwa hao wamesema, msamiati wa msibani unabadilika kwa kiwango kidogo sana kwa sababu shughuli za mazikoni mara nyingi hufanywa na watu wazima na sio vijana, pia msiba umeambatana na mambo ya kidini zaidi ambayo ni vigumu kubadilika.

Pia muktadha wa kilimoni na uvuvini, umeonekana kuwa na kiwango sawa cha mabadiliko kiasilimia sawa na 22.81% kwa kila muktadha. Aidha watafitiwa wamesema miktadha hii aghalabu msamiati wake hubadilika na kuwa na matumizi sawa na Kiswahili sanifu, majina ya mimea ama ya samaki huwa ni vigumu kubadilika miongoni mwa Wapemba wenyewe, aghalabu kubadilika kwa msamiati huo kunatokana na kuingia kitu kipya ikawa tayari kina jina la kigeni, mfano boti, mashine, kebichi na mingineyo.



Kielelezo Na. 4.2: Tathmini ya Mabadiliko ya Msamiati Kiujumla

Kati ya msamiati 57 uliokusanywa, katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni kama ilivyooneshwa huko nyuma. Imedhihirika kuwa msamiati hubadilika katika sura tatu.

1. Upo msamiati uliobadilika kiisimu ambao kwenye msamiati 57 umejitokeza 6 sawa na asilimia 10.53, kama *dunga* - tunga, *kyuo* - chuo, *uili* - uwili, pia *kyambuzi* – kiambuzi, *shaza* - chaza na *shumbwi* – chumbwi. Kipemba cha asili mara nyingi penye herufi ***"ch"*** wakitamka ***"sh"*** mfano ***ch***aza - ***sh***aza, ***ch***ooko - ***sh***ooko, ***ch***ubwi - ***sh***umbwi, ***ch***upa - ***sh***upa na mingineyo.

2. Pia upo msamiati mwingi sana katika mabadiliko umekuwa na maana sawa na Kiswahili sanifu. Kwa mfano, *chunguua* - chunguza, *kukata mahar*i - kudai mahari, *mwanamwari* - mwari, *uchimvi* - uchuro, *agadunia* - kufariki, *tusi* - jeneza, *mava* - makaburi, *hayati* - marehemu, *fufu* - ngombe bahari, *forozani* - bandarini, *chasa* - vusha, *nzuma*ri - mchaichai, *tango* - boga na kadhalika. Hivyo msamiati 46 imegundulika kuwa mabadiliko yake yamekuwa sawa na Kiswahili sanifu, sawa na asilimia 80.70%.

3. Pia upo msamiati ambao umebadika kikawaida katika matumizi, sio kiisimu wala mabadiliko yake haujaenda kwenye Kiswahili sanifu. Umegundulika msamiati 5 kati ya 57 sawa na 8.77%. Mfano; *utu uume* - ujanadume, *adi* - ndwele, *kupamba* - kukafini na *vifiwa* - vizikwa.

4.4 Kuchunguza Sababu Zilizosababisha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati

Malengo maalumu ya tatu yalikuwa ni kuchunguza kwa kina sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni.Watafitiwa kupitia mbinu na zana mbalimbali katika utafiti huu, walikuwa wakijibu swali kuu la tatu la utafiti huu lililokuwa likiuliza; Ni sababu zipi zilizochangia kuleta mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba? Katika kufikia lengo nadharia iliyoanzishwa na Giles (1973), ambayo ilijaribu kutafuta sababu za kuwepo kwa mabadiliko ya wazungumzaji katika mtindo wa matamshi na msamiati mpya wakati wa mawasiliano ya kijamii. Kwa vile miktadha miwili iliyotafitiwa ilihusu mambo ya kijamii (harusini na msibani) na miktadha miwili iligusia mambo ya kiuchumi (uvuvini na kilimoni), hivyo majibu

yaoyameegemea kwenye sababu za kiuchumi na sababu za kijamii. Sambamba na hili watafitiwa walikuwa wakijibu swali kuu la 3 la utafiti huu lililokuwa likiuliza; Ni sababu zipi zilizochangia kuleta mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba? Watafitiwa walieleza sababu hizo na kuzifafanua kama linavyoonesha jedwali na 4.13 kama hapo chini.

Jedwali Na. 4.13: Sababu Zilizosababisha Mabadiliko katika Lahaja ya Kipemba

No	Sababu za Kiuchumi	Idadi	Asilimia	Sababu za Kijamii	Idadi	Asilimia
1.	Biashara	80	89.89%	Kukua kwa sayansi na Teknolojia	87	97.75%
2.	Athari za maendeleo ya watu kuhamahama kwa ajili ya kutafuta shughuli za kuwaendeleza kimaisha	84	94.38%	Mabadiliko ya kiutamaduni	83	93.26%
3.				Msimamo wa kidini	32	35.96%
4.				Matumizi ya utandawazi pamoja na matumizi ya vyombo vya mawasiliano	86	96.63%
5.				Kuwepo kwa lahaja iliyorasmi	85	95.51%
6.				Maingiliano ya Kindoa	82	92.13%

4.4.1 Sababu za Kiuchumi

4.4.1.1 Biashara

Kwa upande wa biashara, watafitiwa 80 kati ya 89 waliohojiwa sawa na 89.89% wameeleza kuwa msamiati mwingi wa Kipemba umebadilika kwa sababu Wapemba wingi hutoka nje ya kisiwa hicho kwa ajili ya biashara. Mfano, mfanya biashara wa Kipemba anaeishi Tanzania Bara ni lazima afuate msamiati wa sehemu hiyo ili apate mawasiliano mazuri katika kufikia lengo lake baina yake na wateja. Kwa mfano, msamiati kama “tungule” atabadili na kuuita “nyanya”, “boga” badala ya “tango”,

“daftari” badala ya “buku”. Pia familia za Wapemba hao zikichanganyika na familia za sehemu ambazo wanaishi hulazimika kubadisha msamiati wao ama kwa kuiga kwa makusudi au bila ya kukusudia na kuacha athari ya kubadilika kwa msamiati wao.

4.4.1.2 Athari za Maendeleo ya Watu Kuhamahama kwa Ajili ya Kutafuta Shughuli za Kuwaendeleza Kimaisha

Watafitiwa 84 kati ya 89 waliojibu swali hili, sawa na 94.38%, walisema kuwa Wapemba wana tabia ya kuhamahama na kuhamia sehemu nyingine kwa lengo la kutafuta njia za kujikwamua kimaisha. Huhamia sehemu zenye rutuba kwa ajili ya kilimo au sehemu zenye masoko ya uvuvi ambapo huendesha shughuli zao za uvuvi. Pia huhamia sehemu ambazo zina miundo mbinu muhimu, fursa nyingine kama vituo vya afya na biashara kama vile maduka, masoko na hata sehemu zinazokubali mifugo. Hivyo utawakuta Wapemba katika nchi mbalimbali wamehamia na hasa za jirani zikiwemo Kenya, Tanzania Bara, Afrika ya Kusini na hata katika mabara mingine, na pia sababu ya usanifishaji wa msamiati ndani ya Kiswahili. Mfano, wa msamiati ambao ukitumika ‘mboji’ kwa sasa Pemba karibia yote wanasema mbolea/samadi, forozani sasa bandarini, kitango pepeta wanasema kitango.

4.4.2 Sababu za Kijamii

4.4.2.1 Kukua kwa Sayansi na Teknolojia

Watafitiwa 87 kati ya 89 sawa na 97.75% wamesema, kutokana na kukua kwa kasi mambo ya sayansi na teknolojia zikiwemo kompyuta, mitandao ya kijamii kama facebook, twiter, whatsap, pia matumizi mbalimbali ya mashine za umeme katika mazingira yaliyowazunguka mfano trekta, friza, feni na kadhalika. Pemba haikuwa

nyuma katika matumizi ya vifaa hivyo na hasa kwa upande wa vijana, wasomi na wafanyabiashara. Msamiati mpya umezuka tena kwa lugha ya kigeni ambayo ni Kiingereza na huwa hauna Kiswahili chake. Mfano facebook, twiter, whatsap na hata kama msamiati huo umejaribu kuundwa ili kupata neno mbadala, unakuwa na matumizi madogo, hata zikichukuliwa hatua za uundwaji wa msamiati mbadala huwa tayari msamiati wa kigeni ushazoeleka miongoni mwa watumiaji hao ambapo huwa ni vigumu kuuzoea msamiati ulioundwa kwa matumizi ya Kiswahili fasaha.

4.4.2.2 Matumizi ya Utandawazi pamoja na Vyombo vya Mawasiliano

Watafitiwa 86 kati ya 89 sawa na asilimia 96.63 wameitaja sababu hiyo, matumizi ya utandawazi pamoja na kukua kwa mawasiliano duniani kote kwa kuwepo vyombo kama simu za mikononi, redio, runinga, magazeti na vyinginevyo. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mabadiliko ya msamiati katika lahaja ya Kipemba. Kutokana na sababu hii, Kipemba kinapata msamiati mpya na kuzoeleka katika jamii, mfano; kachakachua, changamoto, kasheshe, sakata kupitia kwenye magazeti, redio ama runinga. Pia simu za mikononi zinachangia sana kuibua mitindo mipya na hasa katika upande wa isimujamii. Waendelezaji wakubwa wa mtindo huo ni vijana na wasomi ambapo husababisha athari katika lahaja hiyo na hata Kiswahili kwa ujumla. Mfano wa sentensi za Kiswahili za lahaja ya Kipemba zilivyoathiriwa ni utandawazi huo katika mawasiliano ni:

Naizinga nambayo lakini siioni siji **kushaidiliti.**

Naitafuta namba yako lakini siioni sijui **kushaifuta**

Nishahailaiti kazi yangu ela hayetaka **kupestika n-kaisevu.**

Nishaikozesha kazi **yangu** lakini haikutaka **nikaihifadhi**

Msamiati kama hiyo hapo juu, "*kushaidiliti", "nishahailaiti*", *"kupesti", "n - kaisevu", "wasapu"* na *"sijaidaulodi"* ni msamiati watu wanaujua kama ni wa kigeni lakini hawaelewi watumie upi. Wakati mwingine inakuwa ni vigumu kutafuta neno la Kiswahili na hii inasababisha kuchanganya msamiati kwa watumizi ili kurahisisha mawasiliano

4.4.2.3 Mabadiliko ya Kiutamaduni

Pia watafitiwa 83 kati ya 89 wameitaja sababu hii kuwa ni miongoni mwa chanzo kinachosababisha mabadiliko ya msamiati wa Kipemba sawa na asilimia 93.26%. Utamaduni wa Kipemba umebadilika sana. Hii imesababishwa na maendeleo ya kijamii ambayo ndio mfumo wa maisha na hutokea kwa dunia yote. Ni lazima binaadamu abadilike ili aendane na maisha yanayomkabili kwa wakati ule. Binaadamu hawezi kuwa na mila na deturi zilezile kwa kuhofia kubadilisha utamaduni wake.

Mfano, watu wa zamani wakivaa ngozi, huwezi na wewe kwa wakati huu kuvaa vazi hilo ukasema naulinda utamaduni wangu. Utakuwa hupo katika usawa. Miongoni mwa Wapemba walikuwa na utamaduni ambao humlazimisha bi harusi kunyolewa para ili nywele mpya zikaanze kuota akiwa kwake. Lakini kwa sasa haikubaliki. Mambo mapya yametawala kama sherehe ya singo, chai, marusharoho yote hayo husababisha sana kutumia msamiati mpya unaohusu mambo hayo na kuacha au kubadilisha misamiati yao ilimradi waweze kurahisisha mawasiliano miongoni mwao na waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kiulimwengu.

4.4.2.4 Msimamo wa Kidini

Watafitiwa 32 kati ya 89 tu wameona kuwa mambo ya kidini yanasababisha mabadilio ya matumizi ya msamiati wao sawa na 35.96%. Zamani kabla ya watu kuwa na msimamo mkali wa kidini walikuwa wakienda na mila na desturi zao na kujiona wapo sawa tu. Lakini sasa msamiati mwingi wa harusini ama msibani unaotumika ni wa lugha ya Kiarabu kwa vile kisiwa hiki kina waumini wa Kiislamu kwa asilimia kubwa. Mfano akdi (ndoa), hitma, kafini, jeneza na mingineyo. Kwa hiyo watoto wanaanza kuzoea msamiati huo wakiwa wadogo katika madrasa na hugeuka kuwa msamiati wa kawaida kwa jamii zijazo na huwa ni vigumu kutumia msamiati asilia.

4.4.2.5 Kuwepo kwa Lahaja Iliyorasmi

Watafitiwa 85 kati ya 89 sawa na 95.51% wamefafanua kwa kusema, kuwepo kwa lahaja iliyochaguliwa kuwa ni lahaja rasmi katika shughuli zote kuu za kiserikali ikiwemo utoaji wa elimu, mikutano na hata vyombo vya kimahakama ambapo imechangia mabadiliko ya matumizi kwa baadhi ya msamiati wa Kipemba. Hivyo jamii ambayo imeelimika hutumia zaidi lugha rasmi na msamiati yao huiacha kabisa. Vilevile wanafunzi wakiwa vyuoni hutumia lugha rasmi ambapo msamiati wa mjini kukua kwa kiasi kikubwa na ya Kipemba kufa. Ukuaji wa elimu kisiwani humo umesababisha jamii takribani zote kubadili namna yake ya kuzungumza.

4.4.2.6 Maingiliano ya Kindoa

Wahojiwa 82 sawa na 92.13% wamesema sababu hii ya kuoana kati ya Wapemba na jamii nyingine nayo ni miongoni mwa sababu za kubadilika kwa msamiati. Mfano;

Mpemba anapohamia sehemu nyingine na kuishi huko kwa muda mrefu, huoa na kupata watoto. Maingiliano hayo ndio yaliyosababisha msamiati wa harusini kubadilika kuliko msamiati wa muktadha mwingine.

4.5 Muhtasari wa Sura

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili na maelezo. Uwasilishaji huo umezingatia malengo maalumu ya utafiti na umeongozwa na mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Aidha, nadharia za mabadiliko na nadharia kidhi ya mawasiliano imeongoza katika kuchanganua data. Utafiti umefanikiwa kukusanya msamiati wa lahaja za Kipemba ambao unatumika katika muktadha wa harusini, msibani, uvuvini na kilimoni umebadilika kimatumizi. Umeweza kutathmini tofauti ya kiasi cha mabadiliko ya msamiati huo. Mwisho, umeweza kubainisha sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu "Kuchunguza mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba". Sura hii imegawika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti. Sehemu ya tatu inaelezea mapendekezo ya utafiti na sehemu ya nne mtafiti ametoa hitimisho la utafiti kwa ujumla.

5.2 Muhtasari

5.2.1 Muhtasari wa Ujumla

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu ambalo ni "Kuchunguza Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati ya Lahaja za Kipemba katika Muktadha wa Harusini, Msibani, Kilimoni na Uvuvini". Utafiti umefanyika katika vijiji vinne kimoja kutoka kila Wilaya iliyopo Pemba, hivyo utafiti umepata wawakilishi kutoka pande zote za kisiwa hicho.Tasnifu hii imegawanywa katika sura kuu tano kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza, imechambua misingi ya utafiti huu. Mwanzo kabisa imezungumzia usuli wa mada na tatizo la utafiti.Vile vile sura hii imeonesha lengo kuu na malengo maalumu ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti.

Sura ya pili, imejumuisha utalii wa kazi tangulizi kama vitabu, makala, mitandao kuhusiana na mawazo ya wataalamu mbalimbali yaliyolingana na mada ya utafiti pamoja na pengo la utafiti. Pia ndani ya sura hii mkabala wa kinadharia umewekwa.

Zimeainishwa nadharia ya mwenendo na mabadiliko ya Foucault (1998), nadharia ya ubadilikaji ya Darwin (1838) na nadharia Kidhi ya Mawasiliano ya Howard Giles (1973) ambazo zimeuongoza utafiti katika kufikia malengo yake.

Sura ya tatu inahusu mbinu na njia za utafiti. Sura hii nayo imeanza kwa utangulizi mfupi na baadaye ikafafanua njia na mbinu mbalimbali zilizotumika kukusanya taarifa za utafiti. Njia hizo ni njia ya hojaji, usaili na maelezo. Ni katika sura hii imezungumzia mipaka ya utafiti na imepambanua mbinu za usampulishaji wa watafitiwa. Vilevile sura hii imeonesha utaratibu wa ukusanyaji wa data ulivyokuwa pamoja na mbinu za kuchambua na kuchanganua data zilizotumika katika kufikia lengo kuu la utafiti huu na hatimaye ikatoa muhtasari wa sura.

Sura ya nne inahusu uchambuzi wa data. Mwanzo kabisa sura hii imeanza na utangulizi unaohusu uchambuzi huo. Baadaye ikaonesha uchambuzi wake pamoja na matokeo ya utafiti huu kupitia malengo maalumu ya utafiti huu moja baada ya moja na jinsi yalivyofikiwa. Kwanza sura hii ikauainisha msamiati wa harusini, msibani, uvuvini na kumalizia wa kilimoni. Baadaye ikaweka tathmini ya tofauti ya kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia na hatimaye ikaorodhesha sababu zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo

Sura ya tano inazungumzia vipengele vinne. Kipengele cha kwanza kimetoa muhtasari wa utafiti mzima pamoja na muhtasari wa matokeo ya utafiti huu. Mapendekezo ya utafiti yameelezwa katika sura hii na mwisho kabisa utafiti umetoa hitimisho la utafiti kiujumla.

5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Baada ya utafiti kukamilika, matokeo ya utafiti yalipatikana kupitia malengo maalumu matatu ya utafiti kama unavyoonesha hapo chini:

(a) Kuuainisha Msamiati wa Kipemba ambao Umebadilika Matumizi yake katika Muktadha wa Harusini, Msibani, Uvuvini na Kilimoni.

Utafiti huu umebaini kuwa msamiati wa Kipemba upo katika mabadiliko na huko ndiko kukua kwa lahaja hiyo. Ukagundua kuwa mabadiliko ya msamiati huo, kwa kiwango kikubwa huelekea kwenye msamiati wa Kiswahili Sanifu. Matokeo yake ni kama ifuatavyo:

(i) Kipemba ni kimoja tu. Kwani ukiangalia fasili za lahaja; Mfano, Wamitila (2013) amesema lahaja ni lugha zinazotumiwa na kikundi fulani cha watu ambazo huonesha tofauti za maneno (msamiati), umbo, matamshi kwa lugha yenye asili moja. Lakini Kipemba kina msamiati mmoja kwa jamii ya Wapemba wote, maumbo pia yapo sawa katika msamiati isipokuwa Kipemba kina lafudhi nyingi na hasa tukiangalia maana ya lafudhi. Kwa mujibu wa BAKIZA (2012) lafudhi ni utamkaji wa mtu wa maneno ya lugha fulani. Hii ndio inayowasababisha Wapemba kujuana sehemu zao wanazotoka miongoni mwao.

(ii) Kipemba kina sifa ya kuunganisha maneno yake. Inawezekana ikawa kitenzi na kielezi mfano; Usendevyo ikimaanisha usende zako, au nomino na kivumishi mfano; nkonowo - mkono wako. Chungwalo - chungwa lako, vituvyo - vitu vyako.

(iii) Kipemba cha asili na cha ndani kilikuwa maneno yanayoanzia na herufi **"ch"** wanaitamka **"ky"** mfano **ch**uo - **ky**uo, **ch**a - **ky**a, **ch**anda - **ky**anda, **ch**ungu-**ky**ungu, **ch**amchana - **ky**amchana, **ch**eti - **ky**eti. Ingawa matamshi hayo yanabadilika sana.

(iv) Baadhi ya sehemu wanashindwa kutofautisha matumizi ya "**ch"** na badala yake wanaweka "**sh"**. Mfano ku**ch**ota - ku**sh**ota, **ch**o**ch**ea - **sh**o**sh**ea, **ch**aza-**sh**aza, **ch**umvi - **sh**umvi, halikadhalika penye herufi **"sh"** wanaeka **"ch"** kwa mfano; **sh**anuo - **ch**anuo, **sh**avu - **ch**avu, **sh**oki**sh**oki – **ch**oki**ch**oki

(v) Vilevile kuna baadhi ya sehemu za ndani ya Pemba walikuwa wakitumia herufi **"d"** badala ya **"t"** mfano; **d**utu - **t**utu, **d**umbwikia - **t**umbwikia, ku**d**itia - ku**t**itia, **d**unga - **t**unga.

(b) Kutathmini kiasi cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati huo kiasilimia kwa kila muktadha husika.

Matokeo yameonesha kuwa msamiati wa harusini unabadilika kwa kasi kwa asilimia 33.33% ukilinganisa na muktadha wa msibani, kilimoni na uvuvini. Msamiati wa kilimoni na uvuvini unachukua nafasi ya pili katika kasi ya mabadiliko sawa na 22.81% na mwisho ni msamiati wa msibani ambao umeonesha kubadilika kidogo sana sawa na 21.05%. Ingawa msamiati wa msibani, kilimoni na uvuvini haujatofautiana sana kiasilimia katika mabadiliko yake kama ilivyooneshwa hapo juu.

(c) Kuchunguza Sababu Zilizosababisha Mabadiliko ya Matumizi ya Msamiati huo

Watafitiwa wameeleza sababu mbalimbali zilizosababisha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba. Sababu iliyotajwa na watafitiwa wingi ni kukua kwa

sayansi na teknolojia ambapo watafiti 87 kati ya 89 sawa na 97.75% wameitaja sababu hiyo. Kuwepo kwa lahaja iliyorasmi ilishika nafasi ya pili wastani wa wahojiwa 95.51%, Pia kukua kwa utandawazi na vyombo vya mawasiliano ilitajwa kwa kiwango cha 96.93%.

Athari za maendeleo ya watu kuhamahama kwa ajili ya kutafuta maisha, ilizungumzwa na watafitiwa 84 kati ya 89 sawa na 94.38% ikifuatiwa na sababu ya maingiliano ya kindoa kwa wastani wa wahojiwa 92.13%. Sababu ya mabadiliko ya kiutamaduni ilitajwa kwa asilimia 93.26.Pia wahojiwa 89.87% wamesema sababu za kibiashara na watafitiwa wastani wa 35.96% na baadhi ya watafitiwa wameitaja sababu ya msimamo wa kidini ambapo sababu hii ilitajwa na watafitiwa32 sawa na 35.96%

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Msamiati wa Kipemba una nafasi kubwa katika kukiendeleza na kukikuza Kiswahili na pia lafudhi zake zina mvuto kwa Waswahili, kwa hivyo kiendelee kutumika kwani inasaidia kuwatambua watu wenye asili hiyo pamoja na kujaza pengo la istilahi za Kiswahili ili kuepuka kuwa na istilahi za kigeni.

“Kukua kwa Sayansi na Teknolojia” na sababu nyingine zote zilizotajwa kwenye utafiti huu, ambazo zinaweza kuleta athari kubwa itakayosababisha kupotea kwa msamiati wa kilahaja, ili msamiati huo usipotee, ni vyema mtaala wa Zanzibar katika somo la Kiswahili iingize mada ya lahaja katika viwango tofauti kwa lengo la kuziendeleza lahaja za Kiswahii ili ziweleweke na jamii yao na pia jamii nyingine kwani ndio utambulisho wa Wazanzibar na Waswahili kwa ujumla.

Uhifadhi wa msamiati wa lahaja hii ni mdogo sana. Ni vyema wanalughawia na wataalamu wachukue hatua maalumu ya kuuhifadhi msamiati katika kanda, kuandika vitabu pamoja na makamusi na hata kuanzishwa kwa chombo maalumu cha kuhifadhi msamiati wa kilahaja. Pia waandishi wetu hasa wa fani ya fasihi watumie msamiati wa kilahaja ili kulinda lahaja hizi na kuzitangaza kwa jamii mbalimbali za ndani na nje ya Zanzibar ili amana hii ya lugha isipotee.

Vilevile watafiti wingine waendelee na kazi ya utafiti katika nyanja za msamiati wa kilahaja, wachunguze fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantikia pia wanaweza kuendeleza katika muktadha wa shuleni, ofisini, sokoni na miktadha mingine ili kupunguza mwanya wa kitaalamu katika uwanja wa lugha ya Kiswahili. Pia yapo maeneo mingi ya kilahaja ambayo bado hayajatafitiwa yakiwemo mabadiliko ya matumizi ya msamiati katika miktadha mingine kama msamiati wa sokoni, mazungumzoni, mashuleni na hata makazini, tofauti na mfanano wa lahaja ya Kipemba na lahaja nyingine, tofauti ya msamiati katika Kiswahili cha Tanzania Bara na Tanzania visiwani na hasa ikizingatiwa kuwa nchi zote hizo zinatumia mtaala mmoja, tahajia ya Kiswahili kwani kuna mvutano mkubwa miongoni mwa Waswahili wenyewe jinsi ya uandishi kwa baadhi ya msamiati kwa mfano, neno nae - naye, mengine - mingine, hiki- hichi, maua - mauwa, onesha - onyesha na baadhi ya maneno mingi.

MAREJELEO

Abdulaziz, M.H. (1971). *Tanzania National Language Policy and the Rise of Swahili Political Culture, Language in Society 1:197-213.*

Ali, S. Kh. (2007*).* Athari za Usasa katika Lahaja ya Tumbatu Asilia, SUZA.

American Dialect societies (2014), www.americandialect.org. Imepekuliwa tarehe 12/3/2013.

Bakhressa, S.K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*, Oxford University, Nairobi.

BAKITA, (1976). *Lugha Yetu, Tuisome Tuijue, Toleo la 28*, Shirika la Upigaji Chapa Zanzibar.

BAKIZA, (2012*). Kamusi ya Lahaja ya Kipemba***,** Oxford University Press, East Africa Ltd.

BAKIZA, (2012). *Kamusi ya Lahaja ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, East Africa Ltd.

Batibo, H.M. (1982). *The Sourthern Swahili Dealects,* University of Dar-es-salaam.

Chambers J.K and Trudgill, P. (1986). *Dialectology,* CUP Cambridge.

Chiraghdin, Sh. and Mnyampala, M. (1977*). Historia ya Kiswahili*, Oxford University Press, East Africa Ltd.

Chum, H. (1994). *Msamiati wa Pekee wa Kikae (Kae specific vocabulary),* Uppsala Nordin Association.

Denscombo, M. (2005). *The Good Research Guide for Small Scale Social Research Project*, New York: Open University Press.

Enon, C.J. (1998). *Education Research and Measurement, Department of Distance Education,* Makerere University.

Faki, S. Kh. (2011). Affixelements e, ha, and he in Kipemba Dialect, Chuo kikuu Dar-es-Salaam.

Farlex (2003 - 2015). kupitia Mtandao wa *www.thefreedictationary.com/dialects. Imepekuliwa 5/4/2014.*

Foucault, M. (1981). *Language, Counter - Memory Practice*, Ithaca cornell University Press.

Giles, H. (1973). *Accommodition Theory: Communication, Context and Consequence.* New York Cambrige University Press.

Gora, H.H. (2011). Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo, Chuo Kikuu Dodoma.

Haji M.O. (2013). Nafasi ya Hadithi Simulizi katika Kufunza Maadili Mema, Shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar. Chuo Kikuu huria cha Dar-es-salaam.

Haji, G.H. (2006). *Kamusi ya Kitumbatu,* Express Printing Services Zanzibar.

Hamad, S.O. (2011). Tense and Aspect Representation in Standard Swahili and Kipemba, Chuo Kikuu Dar-es-salaam.

Heine, B. (1970). African Languages, An Introduction Cambridge: Cambridge University Press.

Honero, L. N & Sengo T. (1978). *Mulika 12*, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Giles, H. (2010). http://grammar.about.com/od/ab/g/Accommodation.html. Imepekuliwa tarehe 12/1/2014.

Juma, M. A. (2006). Msamiati na Vitenzi katika Lafudhi za Jambiani, Paje, na Bwejuu Katika Lahaja za Kimakunduchi, SUZA.

Juma, M.A. (2011). Ulinganishi wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kizimkazi, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Khamis, A. Salim A. na Kindy N. (1990*). Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kidato Cha Kwanza,* TAKILUKI, Zanzibar.

Khamis, S.A.M. (1984). Urban Versus Rural Swahili (A study of Pemba varieties) Ph.D, Thesis Leipzing.

Khatib, M.S. (2010). *Historia ya Maendeleo ya Kiswahili ZNZ, Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*, TUKI.

Kiango, J.G, Abdulazizi Y.L, Izaac I. na Abdilah N. (2009). *Kamusi ya Shule za Msingi*, Oxford University Press, East Africa Ltd.

Kiango, J.G. (1995*). Kioo cha Lugha, Juzuu 1: Idara ya Kiswahili*, Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*, Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Dar-es-Salaam.

Kipacha, A. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Kothari, C.R. (1985). *Research Methodology*, Wiley Eastern Limited, New Delhi.

Krain, E. (1998). *Agrarian Consitituation of Zanzibar and its Impact on Agricultural Development German*, Born, Wehi

Maganga, C. (1991). *A Study of Morphology of Kiswahili*, Kiunguja, Kipemba, Kimakunduchi and Kitumbatu, Dar-es-Salaam.

Masebo J.A. na Nyangwine, N. (2004). *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili*, Dar-es-salaam: Afro Industries Ltd.

Masebo, J.A na Nyangwine, N. (2007). *Nadharia ya Lugha, Kiswahili 1*, Nyambari Nyangwine Publisher, Dar-es- Salaam./

Massamba, D.P.B. (2007). *Kiswahili Orgins and The Bantu Divergence-Convergence Theory: Insititute of Kiswahili Research*, Dar-es-Salaam, University of Dar-es-Salaam.

Mdee, J.S. (2001*). Makala ya Kongamano ya Kitaifa,* TUKI, Dar-es-salaam.

Mekacha, R. D. K. (1993). *Isimujamii, Nadharia na Muktadha wa Kiswahili.* Osaka Japan.

Mfaume, G.E. (1984). *Misingi ya Isimu ya Lugha ya Kiswahili,* Printpak (T) Ltd Dar-es-Salaam.

Mhilu, G.A. na Masebo, J.A. (2010). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kidato cha Tatu,* Nyambari Nyangwine Publishers Dar-es-salaam, Tanzania.

Mhina, G.A. na Kiimbila J.J. (1971). *Mwalimu wa Kiswahili,* Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.

Mkude, J. S. (1993). *Mtawanyiko wa Lahaja ya Kiswahili TUKI,* Makala za waandishi wa Kiswahili TUKI.

Mlacha, S.A.K. and Hurskainen A. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili, TUKI,* Da-es-Salaam na DAAS Helsi.

Mshindo, H.B. (1988). The Uses of KA in Pemba Swahili Variety, University of Dar-es-Salaam.

Mutiso, K. (1992). Kamusi *ya 1 ya Ushairi wa Kiswahili na Maneno ya Kizamani*, Chuo Kikuu Nairobi.

Mwansoko, H.J. (1992). *Nafasi ya Lahaja katika Kuendeleza Msamiati na Istilahi za Kiswahili Sanifu, makala*.

Nabahany, A. (1995). *Uundaji wa Istilahi katika Lugha ya Kiswahili*, Gologne Germany.

Nurse, D (1982). *A tentative Classification of the Primary Dialects of Swahili in Sprache und Geschichte in Africa* (Vol.4), Hamburg.

Nyangwine N, (2001). *Nadharia ya Lugha Sekondari na Vyuo. Historia, Sarufi, Matumizi, Utungaji na Ufahamu,* Dar-es-salaam, Afroplus Industries Ltd.

O'Grady, W, Debrovolosky M. na Katamba R. (1997).*Contemporary Linguistics An Introduction*, London Longman.

Polome, E.C. (1976). *Swahili Language Handbook,* Washington DC Central for Applied Linguistics.

Ruane, J.M (2005). *Essentials of Research Methods, A Guide to Social Science Research*, Australia, Blackwell Publishing.

Sacleux, C. (1909). *Grammaire des Dialects Swahili***,** Paris Procure des P. Du - Esprit.

Said, D. A. (2011). Viangami katika Kipemba, Chuo kikuu Dar-es-Salaam.

Seidman, I.E. (1991). *Interviewing and Qualitative Research.* A guide for rea.

Sengo, (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi, AERA* Kiswahili Researched Product.

Sengo, T.Y. S. (2011). K*iswahili na Uswahili ni Utambulisho wa Utamaduni na Utaifa,* Alhuda.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*, TUKI.

Simala, I.K. (2002). *Utafiti wa Kiswahili,* Nairobi Moi Universit Press.

Stigand, C.H. (1915). *Grammar of Dialect Changes in the Swahili Language,* Cambridge University.

Taasisi ya Elimu, (1996). *Kiswahili Kidato cha II na III,* Oxford University Press.

Temu, C. (1980). *Lahaja za Kiswahili*, Institute of Kiswahili Research University of Dar-es-salaam.

Tobouret, K. A. (1989). *Seminar D'anthropologic du Languge. MSH. Informations,* Bulletin de la Fondation des Sciences de I'Homme.

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* Kenya Oxford University Press, East Africa Ltd.

TUKI, (2004). *Makala za Semina ya Kitaifa ya Waandishi wa Kiswahili 1, Lugha ya Kiswahili*, TUKI Dar-es-salaam.

TUKI, (2010). Lahaja za Kiswahili, TUKI, Dar-es-Salaam.

Tuli, R.S.K. (1985). *Chimbuko la Kiswahili, Kukua na Kuchimbuka Kwake*, Utalii exporters and Publications.

Tumbo, Z. Masebo J.A. and Mwansoko H.J.M. (1992). *Kiongozi cha Uundaji Istilahi za Kiswahili*, TUKI.

Verschurch P. and Doorewaard H. (2005). *Designing a Research Project*, Publisher Uitgeverij Lemma - The Netherland.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic, London and New York*, Routdige Taylor and Francis Group.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*, English Press Nairobi.

Whiteley, W.H. (1956). *Kimtangata, A Dialect of the Mrima Coast - Tanganyika*, East African Swahili Committee, Makerere Collage Kampala.

Whiteley, W.H. (1958). *The Dialects of Verse of Pemba*, Kampala, East African Swahili Committee.

_____ (1959). *An Introduction to the Rural Dialects of Zanzibar*, University of Dar-es-Salaam.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho I: Maswali ya Hojaji kwa Vijana

Mazungumzo haya yana lengo la kutafuta taarifa kuhusu mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa lahaja za Kipemba katika muktadha wa harusini, msibani, kilimoni na uvuvini. Taarifa zitakazotolewa kwenye mazungumzo haya zitatumika kwa utafiti huu na si vyinginevyo.

Jinsi: Mke ( ) Mume ( ) Nambari ya simu …….

1) Taja msamiati miwili ya kila muktadha husika ambayo unaiona imebadilika, mabadiliko yake pamoja na matumizi.

Muktadha	**Neno la asili**	**Mabadiliko**	**Matumizi**
Mfano	a)Kualisha	a)Kualisa	a)Kuuguza
Harusini	a)…….. b)…….	a)…… b)……	a)…… b)……
Msibani	a)…….. b)…….	a)…… b)……	a)…….. b)……..
Kilimoni	a)…….. b)……..	a)……. b)……	a)…… b)……
Uvuvini	a)…….. b)……..	a)……. b)……	a)…… b)……..

2) Andika msamiati uliosawa na Kiswahili Sanifu pamoja na msamiati uliopoteza matumizi yake wenye asili ya Kipemba.

Muktadha	**Msamiati Uliosawa na Kisw/Sanifu**	**Msamiati Uliopotea**
Mfano	Chicha	Ndanza
Harusini	…… ……..	……. ……...
Msibani	…….. ……..	…… ……...
Uvuvini	…….	……..……

	……..	…….
Kilimoni	…… ……	....…

3) Je, ni muktadha gani wa matumizi ya msamiati wa Kipemba ambao unabadilika haraka Harusini ( ), msibani ( ), kilimoni ( ), uvuvini ( )

4) Toa sababu zilizokufanya uone kuwa mabadiliko sehemu hiyo yanafanyika zaidi.

……

……

5) Je, unadhani ni muktadha upi haupokei mabadiliko haraka kati ya miktadha ya hapo juu. (……..……..)

6) Taja sababu zilizosababisha zisipokee mabadiliko ya matumizi ya msamiati haraka.

……

……

7) Taja mambo yanayochangia mabadiliko ya matumizi ya msamiati ifuatayo:

Harusini: ……...…….……., …….…...

Msibani……..., ……..

Kilimoni……, ……

Uvuvini……..., ……

8) Toa maoni na mapendekezo yako kuhusu ubadilikaji wa msamiati wa Kipemba katika matumizi yake.

……...

.....

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

Kiambatanisho II: Maswali ya Mazungumzo kwa Ajili ya Wazee

Jibu maswali yafuatao kwa mujibu wa upeo wako.

Jinsi: Mke ( ) Mume ( ).

1) Taja msamiati miwili ya kila muktadha husika ambayo unaiona imebadilika na mabadiliko yake.

	Neno la asili	**Mabadiliko**	**Matumizi**
Mfano	Shaza	Chaza	Kiumbe cha pwani jamii ya panga ambacho kina umbo bapa na gamba lake ni gumu sana linaloitwa kombe.
Harusini	a)…… b)……	a)…….. b)……..	a)…… b)……
Msibani	a)…… b)……	a)…… b)……..	a)…… b)……
Kilimoni	a)…… b)……	a)…… b)……	a)…… b)……
Uvuvini	a)…… b)……	a)…… b)……	a)…… b)……

2) Kati ya msamiati wa harusini, msibani, kilimoni na uvuvini ni ipi inayobadilika kwa haraka. ( )

3) Toa sababu zilizokufanya uone kuwa mabadiliko ya msamiati wa sehemu hiyo yanafanyika zaidi na haraka.

……..

……..

4) Je, unadhani ni muktadha upi haupokei mabadiliko haraka kati ya miktadha ya hapo juu. (……..)

5) Taja sababu zilizopelekea zisipokee mabadiliko ya matumizi ya msamiati haraka.

……..……., ……..……,

Harusini ( ), msibani ( ), uvuvini ( ), kilimoni ( ).

6) Taja msamiati uliosawa na Kiswahili Sanifu pamoja na msamiati uliopoteza matumizi yake wenye asili ya Kipemba.

Muktadha	**Msamiati Uliosawa na Kisw/Sanifu**	**Msamiati Uliopotea**
Mfano	Mende	Pepe
Harusini	……. …….	……. …….
Msibani	…….. …….	……. …….....
Uvuvini	……. …….	…….. …….
Kilimoni	…… ……	…….. ……..

7) Je, unahisi mambo yafuatayo yanachangia kupelekea mabadiliko ya msamiati huo. Tia nambari kipi cha kwanza hadi jambo la mwisho na kuacha lililokuwa halihusiki.

- Nyimbo za kizazi kipya na filamu za michezo ya kuigiza ( )
- Mambo ya kidini ( )
- Maendeleo ya sayansi na teknolojia yakiwemo mitandao ( )
- Watu kuwa na elimu ( )
- Uhamaji na uhamiaji ( )
- Wakati na mabadiliko ya zama kimaumbile ( )

8) Taja mambo mengine ambayo hayapo hapo juu lakini unahisi yanayochangia mabadiliko

…….……, ...…….

9) Toa maoni yako kuhusu msamiati wa Kipemba jinsi unavyobadilika katika matumizi.

……

……

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO